



**JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA**

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



**RIPOTI YA JUMLA YA UKAGUZI WA
UFANISI NA WA KIUCHUNGUZI KWA
KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE
31 MACHI, 2012**

**RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA
HESABU ZA SERIKALI**

Machi 2012

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Dira

Kuwa kituo cha ufanisi katika ukaguzi wa hesabu za Serikali na taasisi za umma.

Dhamira

Kutoa huduma ya ukaguzi wa hesabu wenye tija ili kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

Katika kutoa huduma zenye ubora, ofisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:

Uadilifu

sisi ni asasi adilifu inayotoa huduma kwa namna isiyo na upendeleo.

Ubora

sisi ni wanataaluma wanaotoa huduma zenye ubora kwa kuzingatia viwango kubalifu vya ukaguzi

Uaminifu

tunahakikisha tunakuwa na kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala wa sheria.

Mtazamo wa watu

tunatazama na kukazia zaidi katika matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia mteja na kuwa na watumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi.

Uvumbuzi

sisi ni asasi ambayo wakati wote inahamasisha utamaduni wa kupokea na kuendeleza mawazo mapya kutoka ndani na nje ya asasi.

Matumizi bora ya rasilimali

sisi ni asasi inayothamini na kutumia rasilimali za umma ilizokabidhiwa kwa umakini mkubwa.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



Barabara ya Samora, S.L.P. 9080, Dar es Salaam
Telegram: "Ukaguzi", Telephone: 255(022)2115157/8, Fax: 255(022)2117527, E-mail: ocag@nao.go.tz, Website: www.nao.go.tz

Kwa majibu tafadhali taja:

Kumb. Na.....

30 Machi, 2012

Mh. Dkt. Jakaya M. Kikwete,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
S.L.P. 9120,
Ikulu,
Dar es Salaam.

Yah: Kuwasilisha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi na Kiuchunguzi inayojumuisha Taarifa nne (4) za Ukaguzi wa Ufanisi na mbili (2) za Ukaguzi wa Kiuchunguzi

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (iliyorekebishwa 2005) na kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, ninawasilisha kwako ripoti iliyotajwa hapo juu.

Ripoti hii inajumuisha taarifa sita (6) za Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi wa Kiuchunguzi zinazohusisha Serikali Kuu na Serikali za Mitaa itakayowasilishwa Bungeni mwezi Aprili, 2012.

Nawasilisha.

Ludovick S. L. Utouh
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

YALIYOMO

Dibaji	vi
Shukrani	ix
Muhtasari	xi
 Sura ya 1: Tafakari juu ya kaguzi za awali	1
Ukaguzi wa Ufanisi	1
Ukaguzi wa Kiuchunguzi	5
 Sura ya 2: Ukaguzi wa Ufanisi	6
Utangulizi	6
Usambazaji wa maji mijini	8
Matengenezo ya magari ya Serikali	13
Uvunaji wa misitu	17
Mapato ya Serikali za Mitaa yanayokusanywa na wakala	23
 Sura ya 3: Ukaguzi wa Kiuchunguzi	28
Utangulizi	28
Madai ya huduma ya afya kwa Bima ya Afya	30
Ukaguzi Maalum - Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi	34
 Sura ya 4: Mambo yanayohitaji kuzingatiwa	39
Ukaguzi wa Ufanisi	39
Ukaguzi wa Kiuchunguzi	43
 Sura ya 5: Mwelekeo wa kaguzi zijazo	45
Ukaguzi wa Ufanisi	45
Ukaguzi wa Kiuchunguzi	47
 Kiambatanisho	



Dibaji

Ninayo furaha kuwasilisha ripoti yangu ya jumla ya ukaguzi wa ufanisi na ukaguzi wa kiuchunguzi. Ripoti ya ukaguzi wa ufanisi inahusisha ripoti nne za ukaguzi uliofanyika kwenye Serikali Kuu (Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Maji, Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) na kuwasilishwa mbele ya Bunge letu tukufu. Ripoti ya ukaguzi wa kiuchunguzi, kwa upande mwingine, inahusisha ripoti mbili za ukaguzi uliofanyika kwenye Madai ya watoa huduma yahasuyo huduma ya afya zilizotolewa kwa Mfuko wa Bima ya Afya iliyowasilishwa kwa Bodi ya Wakurugenzi, na Ukaguzi maalum wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi iliyowasilishwa kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

Taarifa hii inalenga kuwaeleza wadau wetu (Wabunge, Serikali Kuu na za Mitaa, vyombo vya habari, wafadhili, asasi zisizo za kiserikali, Asasi za Kiraia n.k) muhtasari wa mambo yaliyoonekana kwenye kaguzi za ufanisi na kiuchunguzi zilizotolewa hadi kufikia mwezi Machi 2012. Maelezo zaidi ya muhtasari huu yanaweza kusomwa kutoka kwenye ripoti kamili za ukaguzi zilizotolewa kwa Maafisa Masuuli husika.

Taarifa hii inawasilishwa kwa Rais kulingana na Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kifungu cha 34(1) na (2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma namba 11 ya mwaka 2008.

Chini ya Ibara 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa 2005, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha kwa Rais kila taarifa aliyotoa kufuatana na Ibara ndogo (2) ya Ibara iliyotajwa. Mara taarifa hiyo inapopokelewa, Rais anamwelekeza mtu husika anayetakiwa kuwasilisha taarifa hiyo mbele ya kikao cha kwanza cha Bunge kabla ya siku saba kupita toka kikao cha kwanza cha Bunge kuanza. Ibara hiyohiyo inamruhusu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za

Serikali kuwasilisha ripoti yake kwa Spika wa Bunge iwapo Rais kwa sababu zozote zile atashindwa kuwasilisha ripoti hiyo kwa Spika kama inavyotakiwa kisheria.

Kutungwa kwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya Mwaka 2008 kumeimarisha uhuru wa utendaji kazi wa ofisi yangu katika kutimiza jukumu lake la kikatiba.

Uhuru wa kufanya kazi wa ofisi yangu utaniwezesha kudhibiti matumizi ya rasilimali za ofisi ikiwa ni pamoja na rasilimali watu, fedha ambavyo vitaniwezesha kufanya kazi yangu bila kuingiliwa na mamlaka yoyote.

Sheria hii imepanua mawanda ya ukaguzi kwa kunipa mamlaka kufanya kaguzi za ufanisi (utendaji), uchunguzi, mazingira na ukaguzi maalumu mbali ya ukaguzi wa kawaida wa taarifa za fedha.

Kufuatia kuongezeka kwa mawanda ya ukaguzi, ofisi yangu imetoa taarifa hii ambayo inahusisha taarifa nne za ukaguzi wa ufanisi zilizowasilishwa bungeni na taarifa mbili za ukaguzi wa kiuchunguzi zilizowasilishwa kwenye Bodi ya Wakurugenzi na kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

Kimsingi, taarifa hii imeniwezesha kutoa maoni huru kwa Bunge kuhusiana na matumizi sahihi na uwajibikaji, uwazi na uadilifu katika matumizi ya rasilimali za umma kwenye maeneo ya usimamizi wa usambazaji wa maji, matengenezo ya magari, uvunaji wa misitu, utoaji wa kazi ya ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri kwa wakala, madai ya huduma ya afya yatolewayo na watoa huduma kwa Mfuko wa Bima ya Afya na ukaguzi maalumu Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi. Lengo la kufanya ukaguzi huu wa ufanisi lilikuwa kuangalia kama rasilimali zimetumika vizuri ili kuleta matokeo yaliyotarajiwa kwa kuzingatia uwekevu, tija na ufanisi kama ilivyotarajiwa na kupitishwa na Bunge kwenye maeneo yaliyotajwa.

Ni muhimu kufahamu kwamba wakati ofisi yangu inafanya ukaguzi na kutoa taarifa ya utendaji wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Programu na Mashirika ya Umma na shughuli mbalimbali kulingana na sheria na taratibu

zilizopo, mwisho kabisa wajibu wa kuhakikisha kama kuna ufanisi, uwekevu na tija katika utumiaji wa rasilimali za umma unabakia kwa Maafisa Masuuli. Vilevile ni jukumu la Maafisa Masuuli kuhakisha kuwa yale yaliyojitokeza katika ukaguzi na mapendekezo yaliyotolewa na Mdhibili na Mkaguzi Mkuu yanatekelezwa.

Ni matarajio ya Bunge kwamba Mdhibili na Mkaguzi Mkuu na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi watahakikisha kuwa zipo taarifa za fedha kuhusu usimamizi wa rasilimali za umma katika Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya umma kuhusiana na uwekevu, tija na ufanisi kwenye utekelezaji wa programu mbalimbali. Ofisi yangu inachangia kwa kutoa mapendekezo ili kuboresha utendaji katika sekta ya umma. Kwa jinsi hiyo, Serikali kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma na ofisi yangu zina mchango mkubwa wa kutoa kwa Bunge katika kujenga imani kwa matumizi mazuri ya rasilimali za Umma katika kuchochea maendeleo ya nchi na watu wake. Ingawa majukumu yanatofautiana, matarajio ya usimamizi bora wa rasilimali yanafanana.

Ili kukidhi matarajio ya Wabunge na Umma kwa ujumla Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea kufanya mapitio ya njia bora zaidi za kufanya ukaguzi na kuongeza wigo wa masuala yanayokaguliwa na hivyo kuimarisha utendaji na uwajibikaji katika sekta ya Umma. Aidha, tunahakikisha ukaguzi wetu unalenga na kuyapa kipaumbele maeneo muhimu ili kuchangia katika maendeleo ya sekta ya umma. Kwa kuwa kazi ya ukaguzi ni chachu katika usimamizi wa fedha, tunaendelea kujadili masuala yanayoathiri utawala/uongozi katika sekta ya umma, hasa katika utoaji wa taarifa za usimamizi wa rasilimali na masuala ya utawala bora.

Napenda kutambua mchango wa wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa juhudi kubwa walizofanya katika kutimiza malengo tuliyojipangia licha ya kufanya kazi katika mazingira magumu ambayo ni pamoja na kukosa fedha za kutosha, kukosa vitendea kazi na mishahara duni na wakati mwingine kufanyakazi kwenye maeneo yasiyopitika kirahisi.

Natarajia kuwa Bunge litaona taarifa hii kuwa ni muhimu katika kuiwajibisha Serikali kutokana na jukumu lake la usimamizi wa fedha za Umma na utoaji wa huduma kwa wataanzania. Hivyo nitafurahi kupata mapendekezo ya jinsi gani nitaweza kuboresha taarifa yangu hii kwa siku zijazo.

Ludovick S. L. Utouh
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
S.L.P. 9080,
Dar es Salaam.

30 Machi 2012



Shukrani

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioniwezesha kutimiza wajibu wangu wa Kikatiba wa kutoa taarifa hii ya ukaguzi wa ufanisi na kiuchunguzi. Napenda kumshukuru kila mfanyakazi katika ofisi yangu kwa jitihada zao kuniwezesha kutimiza matakwa ya katiba ya kutoa ripoti ya ukaguzi ufanisi na kiuchunguzi. Nalazimika kuishukuru familia yangu na za wafanyakazi katika ofisi yangu kwa uvumilivu wao wakati wa uandaaji wa taarifa hii.

Napenda kuishukuru Serikali na Bunge kwa kuendelea kuisaidia Ofisi yangu katika kutekeleza majukumu yake.

Vile vile, shukrani za pekee ziende kwa wafadhili hasa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden (SNAO), Serikali ya Sweden kupitia Wakala wa Kimataifa wa Maendeleo wa Sweden (SIDA), benki ya Dunia kupitia programu ya maboresho katika usimamizi wa fedha za umma(PFMRP), wote waliotutakia mema ambao walichangia kwa njia moja au nyingine kwa nia ya kuleta mabadiliko katika ofisi yangu. Mchango wao katika kuendeleza uwezo wa wafanyakazi kiakili, kimfumo wa teknolojia ya mawasiliano na nyenzo mbalimbali vimechangia kwa kiasi kikubwa mafanikio yetu.

Hali kadhalika, ninawashukuru wadau wengine wote ikiwa ni pamoja na Afisa Masuuli wa Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Maji, Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mamlaka za Maji, Mamlaka ya Udhubiti wa Maji na Nishati, Mfuko wa Bima ya Afya na Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi kwa msaada, ushirikiano na kutupatia taarifa muhimu zilizohitajika wakati wa uandaaji wa ripoti.

Shukrani za kipekee ziende kwa wasomi na wataalamu wa kada mbalimbali kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Mzumbe, Chuo Kikuu cha Kilimo, Chuo cha Usafirishaji, wataalamu wa kujitegemea na maafisa wastaafu kwa michango yao ambayo iliboresha ripoti za ukaguzi wa ufanisi kupitia ukosoaji na uhakiki walioufanya katika rasimu ya ripoti.

Napenda pia kutoa heshima kwa Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) ambapo ripoti hizi zitategemewa kujadiliwa. Tunatarajia michango na maagizo yatokanayo na majadiliano ya ripoti hizi kutoka kwa Kamati ya Hesabu za Serikali.

Mwisho, ninapenda kuwashukuru watumishi wote wa umma, Tanzania kote katika Serikali kuu na Serikali za Mitaa bila kuwasahau walipa kodi ambao ripoti hii imewalenga. Michango yao isiyoweza kupimika katika kujenga taifa hatuwezi kukadiria.

Mwenyezi Mungu awabariki wote kama mnavyojitoa katika kusimamia uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma nchini.



Ripoti hii ya ujumla imeanza na tafakari juu ya taarifa za ukaguzi wa ufanisi zilizojadiliwa na Kamati ya Hesabu za Serikali mwezi Oktoba 2011. Taarifa hizi ni kuhusu: Ukaguzi wa Shule, Afya ya Mama wajawazito na Ujenzi wa barabara.

Muhtasari

Katika majadiliano na Kamati ya Hesabu za Serikali, Afisa Masuuli walikubaliana na udhaifu uliooneshwa katika taarifa. Hata hivyo, Maafisa Masuuli hawakuwa wameandaa mipango ya utekelezaji sahihi inayoeleza ni jinsi na wakati gani watatekeleza mapendekezo ya ukaguzi.

Taarifa za ukaguzi wa kiuchunguzi pia zilipokelewa na Bodi ya Wakurugenzi ya Bohari ya Madawa na Idara ya Ushuru na Forodha. Bohari ya Madawa imeanza kufanyia kazi baadhi ya mapendekezo ya ukaguzi. Idara ya Ushuru na Forodha, kwa upande mwingine, bado haijaanza kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa.

Ripoti hii pia inatoa muhtasari wa taarifa nne za ukaguzi wa ufanisi zilizofikishwa mbele ya Bunge letu Tukufu, na ripoti mbili za ukaguzi wa kiuchunguzi. Ripoti moja ya ukaguzi wa kiuchunguzi iliwasilishwa kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mfuko wa Bima ya Afya na ripoti nyingine ya halimashauri Misungwi kwa Katibu Mkuu Kiongozi kwa kuwa matokeo ya ukaguzi huo yaligusa mambo nyeti ya taasisi iliyokaguliwa.

Taarifa ya ukaguzi wa ufanisi inalenga usimamizi wa: Usambazaji wa maji katika maeneo ya mijini; matengenezo ya magari ya serikali; uvunaji wa misitu na utoaji wa kazi ya kukusanya mapato ya Serikali za Mitaa kwa wakala. Ukaguzi wa kiuchunguzi ulilenga madai ya huduma ya afya yatolewayo na watoa huduma kwa Mfuko wa Bima ya Afya na ukaguzi maalum wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi. Masuala muhimu yaliyoripotiwa katika ripoti hizi ni kama ifuatavyo:

Usimamizi wa usambazaji maji mijini

Lengo kuu la ukaguzi huu ni kutathmini utendaji wa Wizara ya Maji na Mamlaka za Maji Mijini katika

kusimamia usambazaji wa maji mijini na kushughulikia masuala ya upotevu wa maji.

Kudhibiti upotevu wa maji ni miongoni mwa majukumu ya Wizara ya Maji, Mamlaka za Maji Mijini na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA).

Tumehitimisha kwamba mfumo wa ufuatiliaji wa usambazaji wa maji mijini hauna ufanisi; ukaguzi wa mtandao unaofanyika hautoshelezi; matengenezo ya kuzuia uharibifu hayapewi uzito; utendaji wa Mamlaka za Maji haufuatiliwi ipasavyo; hatua zinazochukuliwa juu ya mapendekezo yaliyotolewa na EWURA haziridhishi na Wizara ya Maji haijaweka jitihada kubwa kwa Mamlaka za Maji kuhusu mienendo yao katika kukabiliana na upotevu wa maji.

Usimamizi wa matengenezo ya magari ya serikali

Ukaguzi ulilenga kutathmini kama ukarabati na matengenezo ya magari yanayomilikiwa na serikali hufanyika kiuchumi na kiufanisi kwa lengo la kutunza magari na kupunguza matengenezo yasiyo kwenye mpango.

Wizara ya Ujenzi inawajibu wa kusimamia magari ya serikali ikiwa ni pamoja na matengenezo. Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), chini ya Wizara ya Ujenzi inawajibu wa kusimamia matengenezo ya magari ya serikali. Pia wakala anajukumu la kufuatilia gereji binafsi zinazotengeneza magari ya serikali.

Ilihitimishwa kuwa Wizara ya Ujenzi haijaweza kuweka mfumo madhubuti wa usimamizi wa matengenezo ya magari ya serikali. Shughuli za matengenezo ya magari ya serikali hazisimamiwi kiufanisi. Ufuatiliaji wa utendaji wa gereji binafsi na za serikali unaofanywa na TEMESA hautoshelezi.

Usimamizi wa uvunaji wa misitu

Ukaguzi huu umeangalia ufanisi katika vidhibiti vilivyowekwa na Wizara ya Maliasili na Utalii vya

kuhakikisha kwamba mapato yanayotokana na uvunaji wa misitu yanakusanywa kiufanisi ikiwa ni pamoja na kufuatilia utendaji wa vikosi vya doria na vizuia.

Wizara ya Maliasili na Utalii ina wajibu wa kutunga sera na kuweka mikakati itakayowezesha kuwepo kwa usimamizi na uhifadhi endelevu wa maliasili za nchi, na hivyo kuongeza mchango wa sekta katika mapato ya serikali.

Ilihitimishwa kwamba udhibiti uliowekwa na Wizara ya Maliasili na Utalii dhidi ya ukusanyaji wa mapato yatoanayo na uvunaji wa misitu ya serikali kuu haufanyi kazi yake vizuri. Zaidi ya hayo, Wizara ya Maliasili na Utalii haijaweza kufuatilia utendaji wa vizuia na vikosi vya doria katika kushughulikia tatizo la uvunaji na biashara haramu.

Usimamizi wa kazi ya ukusanyaji wa mapato ya halmashauri iliyotolewa kwa wakala

Madhumuni ya ukaguzi huu ni kuchunguza kama kazi ya ukusanyaji wa mapato ya halmashauri iliyotolewa kwa wakala inasimamiwa kiufanisi na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Pia, kuangalia kama taratibu zitumikazo kuwapata wakala zinafuatiliwa na kutathminiwa ipasavyo na Ofisi ya Waziri Mkuu-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI).

OWM - TAMISEMI inawajibu wa kusimamia fedha za Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na utoaji wa msaada wa kiufundi, uwezo na ufuatiliaji wa Serikali za Mitaa katika ukusanyaji wa mapato yao.

Ilihitimishwa kwamba halmashauri hazifanyi maamuzi madhubuti kabla ya kuamua kuwapa wakala kazi ya ukusanyaji wa mapato ya halmashauri zao; utaratibu unaotumika kuwapata wakala hauna uwazi na haufanyiki kiufanisi; mikataba hailindi maslahi ya halmashauri; ufuatiliaji wa ukusanyaji wa mapato yanayokusanywa na wakala unaofanywa na halmashauri hauna ufanisi.

Madai ya watoa huduma ya afya kwa Mfuko wa Bima ya Afya

Lengo la ukaguzi huu ni kuangalia kama kuna udanganyifu katika mchakato wa kuandaa na kulipa madai ya watoa huduma za afya yanayopelekwa Mfuko wa Bima ya Afya.

Mfuko wa Bima ya Afya unawajibu wa kuwahakikishia wanachama wake upatikanaji wa huduma za matibabu. Uendeshaji wa Mfuko wa Bima ya Afya unaongozwa na sheria na kanuni ambazo zinatoa taratibu juu ya uandikishaji wa wanachama, ukusanyaji wa michango na utoaji wa huduma ya afya kwa wanachama wake.

Ilihitimishwa kuwa mfumo uliopo haukuweza kubaini wanachama batili waliopatiwa huduma ya afya katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Mfuko wa Bima ya Afya una udhibiti dhaifu katika madai ya maabara yanayotolewa na watoa huduma; taratibu zinazotumika katika utoaji wa dawa zina udhaifu katika udhibiti; mfumo wa kusimamia taarifa za wanachama haufanyikazi kiufanisi.

Ukaguzi maalum Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi

Lengo la ukaguzi maalum ni kutathmini usimamizi wa mapato na matumizi katika eneo la uuzaji wa mali chakavu, mishahara, akaunti za benki, miradi ya maji vijijini, Programu ya maendeleo ya kilimo ya Wilaya, Programu ya uwekezaji katika sekta ya kilimo ya Wilaya, ujenzi wa jengo la makazi ya Mkurugenzi na la ofisi ya halmashauri ya Wilaya, masurufu ambayo hayajarejeshwa, mahusiano na migogoro kazini.

Miongoni mwa mambo yaliyoonekana katika ukaguzi ni malipo ya kughushi ya thamani ya Shilingi 43,668,000; mishahara ambayo haijadauiwa na haijawasilishwa Hazina ya Shilingi 24,581,698; Udhaifu katika ukusanyaji wa mapato (Shilingi 7,117,500 zilizokusanywa lakini hazijawasilishwa kwa mtunza fedha); Ukosefu wa udhibiti wa malipo kwa hundi; kutofuata Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na Kanuni zake; usimamizi dhaifu wa idara ya afya; Ukosefu wa usimamizi sahihi katika

miradi ya ujenzi na uhamishaji wa fedha usiofuata taratibu Shilingi 63,680,000.

Udhaifu unaonesha kuna usimamizi dhaifu katika uuzaji wa mali chakavu, mishahara, akaunti ya benki, miradi ya maji, miradi ya kilimo, miradi ya ujenzi na mahusiano kazini.

Ripoti hii ya jumla ya ukaguzi na taarifa kamili husika ya ukaguzi inaweza kutumiwa na kamati ya Bunge katika majadiliano na Maafisa Masuuli juu ya hatua zilizochukuliwa kushughulikia udhaifu ulioonekana.

Sura ya Nne ya ripoti hii inatoa muhtasari wa masuala ambayo yanahitaji Serikali kuyaangalia kwa makini kwani yametokea zaidi katika kaguzi zilizofanyika hadi sasa. Masuala hayo ni: udhaifu katika ufuatiliaji, tathmini, miongozo, mawasiliano, takwimu, hatua zinazochukuliwa kutokana na taarifa zilizopokelewa kutoka ngazi ya chini na usimamizi wa muda katika utoaji wa huduma. Vile vile, udhaifu katika mazingira ya udhibiti, tathmini ya vihatarishi, mwongozo kwa ajili ya kuzuia udanganyifu, ubadhirifu wa mkataba yameonekana katika ukaguzi wa kiuchunguzi.

Serikali inatakiwa kuhakikisha kwamba ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za serikali katika ngazi mbalimbali zinafanyika kiufanisi. Mawasiliano yanaboreshwa na hatua sahihi zinachukuliwa kutokana na ripoti zilizowasilishwa.

Ripoti hii pia inaeleza mwelekeo wa ukaguzi wa ufanisi na kiuchunguzi katika kipindi kijacho. Katika ukaguzi wa ufanisi, kaguzi zijazo zitalenga bajeti, usimamizi wa mikataba, mazingira na utoaji huduma unaofanywa na serikali.

Katika ukaguzi wa kiuchunguzi, mlengo utakuwa kwenye maeneo yenye udhaifu yaliyoonekana zaidi katika kaguzi zetu maalum za karibuni. Hii ni pamoja na, uchunguzi wa kuwepo kwa njama wakati wa kuingia mkataba, ubadhirifu wa mali, ulaghai katika hundi na matumizi mabaya ya ofisi.



Ukaguzi wa Ufanisi

Sura ya 1

Tafakari juu ya kaguzi za awali

Maamuzi kutoka ripoti za kaguzi zilizopita

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hadi sasa ameshatoa ripoti kumi na moja za Ukaguzi wa Ufanisi. Katika ripoti hizo, ripoti moja ilitolewa mwaka 2007, ripoti nne (2010), ripoti mbili (2011) na ripoti nne (Februari 2012). Ripoti zilizowasilishwa miaka ya nyuma zinahusu: Usimamizi wa kuzuia na kupunguza athari za mafuriko, ukaguzi wa shule za sekondari, usimamizi wa huduma ya afya ya msingi, usimamizi wa taka ngumu katika miji mikubwa na manispaa, utayarishaji wa mafao ya wastaafu, ujenzi wa barabara na usimamizi wa huduma ya afya kwa mama wajawazito. Ripoti zilizowasilishwa katika mwaka huu wa 2012 zinahusu Usimamizi wa usambazaji maji maeneo ya mijini, usimamizi wa matengenezo ya magari ya serikali, usimamizi wa mapato yatokanayo na uvunaji wa misitu na usimamizi wa kazi za ukusanyaji mapato ya Halmashauri zilizotolewa kwa mawakala.

Mnamo Oktoba 2011, ripoti tatu za ukaguzi wa ufanisi zinazohusu huduma ya afya ya mama wajawazito, ukaguzi wa shule na ujenzi wa barabara ziliwasilishwa kwa Kamati ya Hesabu za Serikali kwa majadiliano. Hii ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Kamati ya Hesabu za Serikali kujadili ripoti za ukaguzi wa ufanisi tangu ofisi imetoa ripoti ya kwanza mwaka 2007. Ripoti zilizojadiliwa zilikuwa na malengo yafuatayo:

Huduma ya afya kwa mama wajawazito: kutathmini kama mfumo wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wa kufuatilia, kutathmini, kutoa elimu ya afya ya uzazi na mgao wa fedha kwa ajili ya

shughuli zinazohusiana na huduma za afya kwa mama wawawazito unafanya kazi kiuchumi na kiufanisi.

Ukaguzi wa shule za sekondari: kutathmini kama Idara ya Ukaguzi wa Shule za Sekondari katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inatimiza lengo lake la kulinda uhakika wa ubora wa mafunzo katika shule za sekondari. Ukaguzi ulilenga kuchunguza kama ukaguzi wa shule unashughulikia ipasavyo tatizo la matokeo mabaya ya wanafunzi katika shule za sekondari kwa kutumia rasilimali zilizopo.

Ujenzi wa barabara: kutathmini kama Serikali, kupitia Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara Tanzania wana mfumo madhubuti wa kusimamia kazi za barabara nchini. Hii inahusisha kutathmini kiwango cha mfumo kufanya kazi na kupunguza ucheleweshaji, kuongezeka kwa gharama na matatizo ya ubora wa kazi za barabara.

Majadiliano yalikuwa na mafanikio. Maafisa Masuuli walikubaliana na udhaifu uliotajwa katika ripoti ya ukaguzi. Hata hivyo, Maafisa Masuuli hawakuwasilisha mipango ya utekelezaji ili kukabiliana na udhaifu ulioonekana. Majibu yaliyotolewa yalikuwa ya kinadharia zaidi na siyo ya vitendo. Kwa kawaida mipango ya utekelezaji inaonesha ni jinsi na wakati gani mkaguliwa amepanga kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kuboresha udhaifu ulioonekana. Mpango wa utekelezaji ndiyo msingi wa majadiliano wa ripoti za ukaguzi wa ufanisi. Vile vile, mpango wa utekelezaji hutumiwa na Mdhambi na Mkaguzi Mkuu kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa. Maafisa Masuuli waliagizwa kuandaa

mipango ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Mdhambi na Mkaguzi Mkuu kama ifuatavyo:

Huduma ya Afya kwa Mama Wajawazito:

Afisa Masuuli aliagizwa kuandaa mpango wa utekelezaji kuhakikisha kuwa:

- Wizara inafuatilia ipasavyo huduma ya afya kwa mama wajawazito nchini,
- mwongozo toshelezi unatolewa kwa vituo vya huduma ya afya juu ya elimu ya afya ya uzazi inayopaswa kutolewa kwa wananchi,
- Wizara inatathmini mara kwa mara vipengele muhimu vya afya vinavyohusiana na huduma ya afya ya uzazi,
- kunakuwepo na kielelezo sahihi cha bajeti katika kutenga fedha kwa ajili ya afya ya uzazi.

Mpango wa Ukaguzi wa Shule za Sekondari:

Afisa Masuuli aliagizwa kuandaa mpango wa utekelezaji kuhakikisha kuwa:

- kuna vipaumbele vya wazi katika mipango ya ukaguzi wa shule,
- tatizo la wanafunzi wenye matokeo dhaifu linashughulikiwa ipasavyo wakati wa ukaguzi wa shule,
- taarifa ya matokeo ya ukaguzi wa shule inapelekwa pia kwa wadau wote na ufuatiliaji na tathmini ya mapendekezo ya ukaguzi wa shule unafanyika kwa ufanisi.

Ujenzi wa Barabara

Afisa Masuuli aliagizwa kuandaa mpango wa utekelezaji katika:

- kutatua matatizo ya ucheleweshaji, ongezeko la gharama na ukosefu wa ubora katika miradi ya ujenzi wa barabara,

- kufuatilia sababu za ucheleweshaji, ongezeko la gharama na matatizo ya ubora katika miradi ya barabara.
- kuanzisha mifumo bora ya kazi ya kushughulikia ucheleweshaji, kuongezeka kwa gharama na matatizo ya ubora katika ujenzi wa barabara.
- kushirikisha timu huru ya mradi wa ujenzi wa barabara itakayofanya kazi yake kitaaluma na kiuadilifu katika kushauri Wakala wa Barabara jinsi ya kuwapata na kufuatilia washauri.

Ukaguzi wa Kufuatilia

Kama njia ya kukamilisha mzunguko wa ukaguzi wa ufanisi, masuala au mapendekezo ambayo yaliwasilishwa katika taarifa zilizopita na yana umuhimu, ni lazima yafanyiwe ukaguzi wa ufuatiliaji. Lengo la ukaguzi wa ufuatiliaji ni kuangalia kama matatizo yaliyoonekana awali yametatuliwa au la. Masuala yanaweza kubadilika kulingana na wakati; kulenga tu kwenye hatua madhubuti zilizochukuliwa katika kila pendekezo kunaweza kusitoe picha halisi ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwani mapendekezo mengine yanaweza yasihusike kutokana na mabadiliko yaliyotokea.

Madhumuni ya ukaguzi wa ufuatiliaji ni kuangalia maboresho yaliyofanyika katika kushughulikia udhaifu ulioonekana. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepanga kufuatilia mapendekezo yaliyotolewa, na taarifa yake itatolewa katika ripoti ijayo ya jumla ya ukaguzi wa ufanisi.

Matarajio kutoka Bungeni

Tunatarajia Bunge letu Tukufu, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Spika, litajadili ripoti nane zilizobaki kwa lengo la kuchochea uwajibikaji na maboresho katika Wizara, Idara, Wakala, Serikali za Mitaa na mashirika ya umma watumiaipo rasilimali za umma kutoa huduma kwa wananchi.

Ukaguzi wa Kiuchunguzi

Hatua zilizochukuliwa kutokana na taarifa za Ukaguzi zilizopita

Taarifa mbili za awali za Ukaguzi wa kiuchunguzi ziliwasilishwa Bungeni mwezi Aprili 2011, kupitia taarifa ya jumla ya Ukaguzi wa thamani ya Fedha na Ukaguzi wa kiuchunguzi. Taarifa zilijumuisha; Ukaguzi uliohusu Udhibiti wa Mifumo ya Ndani wa Idara ya Forodha ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na; Ukaguzi wa kutathmini uwezekano wa kutokea vitendo vya ubadhirifu na udhibiti wa tuhuma zinazohusu udanganyifu katika Idara ya Bohari ya Madawa (MSD).

Kaguzi hizi mbili za kichunguzi zililenga kuangalia udhibiti uliowekwa na taasisi husika kwa lengo la kutathmini kama udhibiti uliopo ndani ya taasisi hizo una uwezo wa kukabiliana na vitendo vya udanganyifu. Taarifa husika ziliwasilishwa kwenye Bodi za Wakurugenzi ili zifanyiwe kazi na kuhakikisha utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi.

Kama sehemu ya hatua za kufanyia kazi mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Bodi ya Wakurugenzi ya MSD kupitia Menejimenti:

- Imeunda kitengo cha 'Risk Management' kinachoratibu na kuainisha vihatarishi, kuchambua, kutathmini na kutoa taarifa za masuala yenye vihatarishi vya ubadhirifu kwa Menejimenti, Kamati ya Tathmini na Ukaguzi wa Vihatarishi ya Bodi kwa kutumia rejista ya vihatarishi juu ya vitendo vya ubadhirifu ndani ya taasisi.
- Imeagiza kitengo cha ukaguzi wa ndani kupitia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za usimamizi na udhibiti wa vihatarishi vya ubadhirifu.

Menejimenti ya MSD bado haijaanzisha mwongozo katika shughuli za uchunguzi kwa mujibu wa mapendekezo ya

ukaguzi. Juhudi zaidi zinahitajika ili kuanzisha mwongozo huo katika siku zijazo.

Vilevile, Idara ya Usimamizi wa Forodha na Ushuru haikufanya tathmini juu ya vihatarishi vya ubadhirifu kwa ajili ya kudhibiti udanganyifu katika shughuli zake. Mapendekezo ya kutekeleza mpango wa mabadiliko ya mzunguko wa kazi uliopo kwa ajili ya Mamlaka ya Mapato na uanzishwaji wa taratibu za udhibiti zilizozingatia utendaji wa mtu binafsi na ule wa kundi una haja ya kuzingatiwa.



Sura ya 2

Ukaguzi wa ufanisi

Utangulizi

Madhumuni ya Ukaguzi

Ukaguzi wa Ufanisi una malengo ya Kuteka mawazo (*drawing attention*) katika vikwazo vinavyozuia ufanisi na tija katika matumizi ya rasilimali kwenye sekta ya umma; Kutoa misingi ya maamuzi ya kisera yahusuyo kuendeleza ufanisi kwa ajili ya matumizi ya Bunge, wizara, idara, taasisi za serikali, serikali za mitaa na mashirika ya umma; Kutoa taarifa kwa Bunge, wizara, idara, taasisi za serikali, serikali za mitaa na mashirika ya umma zitakazowezesha kutekeleza mapendekezo yatakayoongeza ufanisi; Kuwapa moyo viongozi katika sekta za umma ili waanzishe mchakato wa kutoa taarifa juu ya utendaji wao ili kuchangia katika kuongeza uwajibikaji.

Mamlaka ya Ukaguzi

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Tanzania ana mamlaka ya kisheria ya kufanya ukaguzi wa ufanisi kupitia Sheria ya Ukaguzi ya Na. 11 ya mwaka 2008. Kifungu cha 28 cha Sheria hii kinasema “*Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa lengo la kuthibitisha uwekevu, tija na ufanisi katika matumizi ya fedha au rasilimali za taasisi za umma, anaweza kukagua, kuchunguza na kutoa ripoti, kadiri atakavyoona inafaa, juu ya:*

- a) Matumizi ya fedha na rasilimali za umma katika wizara, idara, mamlaka za Serikali za mitaa na mamlaka nyingine za serikali;*
- b) Utekelezaji wa majukumu ya maafisa masuuli, wakuu wa idara na wakuu wa taasisi mbalimbali za umma;*

- c) *Utekelezaji wa matakwa ya sheria, kanuni, sera na viwango mbalimbali vinavyohusu utunzaji wa mazingira*”

Viwango vya Ukaguzi

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi (INTOSAI), Shirika la Taasisi Kuu za Ukaguzi za Mataifa ya Afrika (AFROSAI) na Shirika la Taasisi Kuu za Ukaguzi za Mataifa ya Afrika ya Nchi zinazozungumza Kingereza (AFROSAI-E). Kuwa mwanachama wa mashirika ya kimataifa, Ofisi ina wajibu wa kuzingatia mahitaji ya viwango vya INTOSAI.

Ukaguzi unafanyika kwa mujibu wa viwango vya ukaguzi wa ufanisi. Viwango hivyo vinahitaji timu ya ukaguzi kupanga na kutekeleza ukaguzi ili kupata ushahidi wa kutosha na sahihi wa kutoa msingi unaofaa wa matokeo na hitimisho kulingana na lengo la ukaguzi. Timu ya ukaguzi inaamini kwamba ushahidi uliopatikana unatoa msingi unaofaa wa matokeo na hitimisho kwa kuzingatia lengo ukaguzi.

Lengo la Ripoti hii ya Jumla

Ripoti hii ya jumla inalenga kuwapa taarifa muhimu Waheshimiwa Wabunge, vyombo vya habari, umma pamoja na wadau wengine zitakazowasaidia kufanya maamuzi yakayoongeza uwekevu, tija na ufanisi. Ili kufanikisha hili, muhtasari wa kila ripoti umehitimishwa na ujumbe kwa Kamati ya Bunge unaohusu masuala ambayo wanaweza kuyahoji kwa Maafisa Masuuli.

Ripoti hii haikusudii kuwa mbadala wa ripoti tano ambazo zimeelezwa kwa muhtasari katika sura zinazofuata. Ili kuweza kupata uelewa zaidi juu ya matokeo ya ukaguzi kwa ajili ya kuwahoji maafisa

masuuli katika maeneo husika, msomaji anashauriwa kusoma ripoti kamili.

Uthibitisho juu ya Uhakika wa Taarifa

Wizara, Idara na Wakala waliokaguliwa walipewa nafasi ya kupitia na kutoa maoni yao katika kila ripoti kwa nia ya kuthibitisha usahihi wa matokeo hayo. Maoni hayo yalizingatiwa wakati wa kukamilisha ripoti hizi.

Muundo wa Ripoti

Sura hii ina muhtasari wa ripoti nne za ukaguzi wa ufanisi zinazoelezea kilichochunguzwa, Kwanini ni muhimu, tulichokiona, hitimisho na masuala ya kujadiliwa na Maafisa Masuuli. Ripoti tajwa ni kama ifuatavyo: Usimamizi wa usambazaji maji maeneo ya mijini, usimamizi wa matengenezo ya magari ya serikali, usimamizi wa mapato yatokanayo na uvunaji wa misitu na usimamizi wa kazi za ukusanyaji mapato ya Halmashauri.



Usimamizi wa Usambazaji wa Maji katika maeneo ya Mjini

Tulichochunguza

Serikali ya Tanzania inatoa huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na usambazaji wa maji safi na ukusanyaji wa majitaka. Huduma hizi zinaathiri ustawi wa jamii nchini kote. Wizara ya Maji, Mamlaka ya Udhhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) na Mamlaka za Maji Mijini zina wajibu wa kusimamia utoaji wa huduma hizi kwa mujibu wa malengo yaliyowekwa, miongozo na taratibu zilizopo.

Katika ukaguzi huu, tulichunguza utendaji wa Wizara ya Maji, EWURA na Mamlaka za Maji Mijini katika kudhibiti upotevu wa maji. Lengo lilikuwa kutathmini kama utendaji wa Mamlaka za Maji Mijini katika kusimamia usambazaji wa maji mijini ulizingatia kikamilifu kushughulikia suala la upotevu wa maji. Pia tulichunguza shughuli za ufuatiliaji uliofanywa na Serikali Kuu (EWURA na Wizara ya Maji) kwa lengo la kutathmini kama unatosha kukabiliana na tatizo la upotevu wa maji.

Ukaguzi uliangalia mambo yaliyotokea katika kipindi cha miaka mitatu tangu Julai 2007 hadi Juni 2010. Takwimu juu ya usimamizi wa mfumo wa usambazaji maji zimekusanywa kutoka Mamlaka 8 za Maji Mijini kati ya 20 zilizoko nchini kote. Utendaji wa EWURA na Wizara ya Maji pia uliangaliwa kwa sababu ya majukumu yao kama wadhhibiti na watunga sera katika sekta ya maji.

Umuhimu wake

Huduma ya usambazaji maji nchini inakabiliwa na matatizo mengi. Miongoni mwa matatizo hayo ni huduma kuwafikia watu wachache, kiwango duni cha huduma, na maji kukatika mara kwa mara. Pia mara

kwa mara mabomba hupasuka na kuvuja hivyo kuathiri wingi wa maji yanayowafikia watumiaji.

Katika mwaka wa fedha 2008/2009, jumla ya kiasi cha maji yaliyopotea katika Mamlaka zote za maji mijini ilikuwa ni zaidi ya 44%. Hii ina maana kuwa karibu nusu ya maji yaliyozalishwa yalipotea kabla ya kufikia wateja na/au hayakuwekwa kwenye bili za wateja. Upotevu wa Maji kwa sababu ya kuvuja, wizi, wateja kutopelekewa bili au kupewa bili zilizo pungufu, au udhibiti mbaya wa mfumo, hupelekea hasara ya kifedha kwa jamii.

Miradi mingi ya maji hugharimu fedha nyingi hivyo kuna haja ya kuweka sawa kumbukumbu, usimamizi mzuri na uwajibikaji. Kuzalisha maji na kupotea hadi asilimia 50% ni kupoteza fedha za walipa kodi. Katika nchi zilizoendelea kwa mfano Ujerumani, Maji Yasiyoleta Mapato (*Non Revenue Water*) hayazidi 5%. Katika nchi zinazoendelea kama Tanzania, kikomo cha kitaifa cha upotevu wa maji kilichowekwa ni 20%. Kwa hiyo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliamua kufanya ukaguzi wa ufanisi uliolenga usimamizi wa upotevu wa maji (ambao hujulikana kama Maji yasiyoleta Mapato) katika maeneo ya mijini.

Tulicho- kibaini

Kwa miaka mitatu mfululizo iliyoangaliwa katika ukaguzi huu hapakuwa na mafanikio makubwa katika kupunguza upotevu wa maji katika Mamlaka za Maji zilizokaguliwa. Mamlaka zote zilijiwekea lengo la upotevu wa maji lililo chini ya lile lililowekwa na Wizara ya Maji la 20%.

Nusu ya mamlaka za maji zilizopitiwa katika ukaguzi huu zimefanya uchambuzi wa sababu za upotevu wa maji na kuandaa mikakati ya kupunguza. Hata hivyo,

mikakati hiyo haikuambatana na mipango ya utekelezaji pamoja na viashiria maalumu vya utendaji ambavyo vinaweza kutumika katika kufuatilia utendaji.

Mamlaka za maji hazijafanya ukaguzi makini juu ya utendaji wa mitandao yao yote ya usambazaji maji.

Taarifa za kuvuja maji ambazo hutokea baada ya saa za kazi, siku za mwisho wa wiki na siku za sikukuu hazikurekodiwa. Hakuna taarifa zinazoonesha muda unaotumika katika kushughulikia uvujaji. Mara nyingi, inachukua zaidi ya saa 24 tangu uvujaji unaporipotiwa hadi matengenezo yanapofanyika.

Pamoja na kwamba nusu ya mamlaka za maji zilizokaguliwa zimeweka simu za bure kwa ajili ya kupokea taarifa kutoka kwa wateja juu ya uvujaji, siyo simu zote zimekuwa zikifanya kazi wakati wote.

Mamlaka za maji hazikutenga bajeti tofauti kwa ajili ya shughuli za ukarabati kama inavyoelekezwa na miongozo. Badala yake gharama za ukarabati zimekuwa zikichanganywa na gharama za matengenezo ya kawaida.

Hakuna timu rasmi au kitengo kinachoweza kuthibitisha ubora wa vifaa vinavyotumika kutengeneza mitambo ya mitandao ya maji.

Wakala nyingi za Maji Mijini (UWSSAs) hazina mita za kutosha za kupimia maji ili kuweza kubaini ni dosari gani inachangia uvujaji wa maji na kwa kiasi gani. Hivyo, kushindwa kujua hasa ni wapi, na vipi na kwa nini maji yanapotea na kwa kiasi gani kwa kila eneo. Pia Mamlaka za Maji Mijini hazijui kila kasoro inachangia kiasi gani cha uvujaji

Mamlaka (3) kati ya Mamlaka (8) za maji zilizokaguliwa zilibainika kutokuwa na mita za kupimia maji kwa wateja. Hivyo, kiasi cha ankara za maji zinazotolewa kwa wateja ni za makadirio ambazo zinaweza kuwa na makosa na kusabisha hasara kwa mamlaka.

Mapendekezo yaliyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) kwa Mamlaka za Maji (UWSSAs) kuhusu kupunguza upotevu wa maji hayakutekelezwa.

Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) mara chache hutembelea Mamlaka za Maji (UWSSAs) kwa lengo la kuhakiki takwimu zinazowasilishwa kwao kuhusiana na uvujaji wa maji (NRW). Aidha, Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) huwa haifanyi ufuatiliaji ili kuona kama mapendekezo yaliyotolewa kwa mamlaka za maji yanatekelezwa na Mamlaka husika.

Kwa wastani, Mamlaka za Maji Mijini (UWSSAs) hupoteza mapato ya jumla ya Sh. Bilioni 2.5 kila mwezi kutokana na maji yanayopotea.

Hitimisho

Ufuatiliaji wa mfumo wa usambazaji maji hauna ufanisi. Ukaguzi wa mitandao ya maji haukafanywa vya kutosha. Matengenezo ya mitandao iliyoripotiwa kuvuja haikutekelezwa kwa ufanisi kwa vile udhibiti wake ulichukua zaidi ya saa 24 tangu taarifa za uvujaji zitolewe kwa Mamlaka husika. Matengenezo ya kuzuia uharibifu hayakupewa uzito. Utendaji wa mamlaka za maji haukufatiliwa kwa ufanisi. Hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa na Mamlaka za Maji Mijini kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na

Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA).

Aidha, Wizara ya Maji haijachukua jitihada za kutosha kuongeza msukumo zaidi ili kukabiliana na upotevu wa maji.

**Masuala
ya
kuzungu-
mza na
Maafisa
Masuuli**

Muhtasari wa ripoti ya ukaguzi na ripoti kamili ya ukaguzi wa utendaji juu ya usambazaji maji inaweza kutumiwa na Kamati ya Bunge zinazosimamia Hesabu za Serikali au kamati za kisekta zinazohusika na kusimamia Mamlaka za maji kuwahoji Maafisa Masuuli juu ya hatua zilizochukuliwa katika masuala yaliyobainishwa kama ifuatavyo:

- i) Kupunguza kiwango cha uvujaji wa maji (NRW) kwa Mamlaka zote za Maji (UWSSAs) ili kuweza kufikia lengo lililowekwa ambalo ni asilimia ishirini.
- ii) Uchanganuzi wa sababu za uvujaji wa maji (NRW), kuweka mikakati ya kupunguza uvujaji wa maji (NRW), kutekeleza mikakati iliyowekwa na ufuatiliaji wake. Pia itathmini utendaji wa mikakati hiyo.
- iii) Kufanya ukaguzi wa makini juu ya utendaji wa mitandao ya usambazaji maji.
- iv) Kuhakikisha muda wa kushughulikia uvujaji unashughulikiwa kwa wakati.
- v) kuweka kipaumbele katika matengenezo ya kuzuia uharibifu.
- vi) Kuboresha ubora wa vifaa vinavyotumika kwa ajili ya shughuli za ukarabati na matengenezo ya mitandao ya maji.
- vii) Kufunga vifaa sahihi vya kupimia maji kama mita kubwa (bulk meters) na mita za wateja kwa lengo la kubaini hasa ambapo uvujaji wa maji hutokea.

- viii) kutekeleza mapendekezo yanayotolewa na Mamlaka ya Udhiditi Nishati na Maji (EWURA) kwa Mamlaka za Maji (UWSSAs) kuhusu kupunguza uvujaji maji (NRW).

Ripoti hii pia inaweza kutumiwa kuuliza Maafisa Masuuli wa EWURA pamoja na Wizara ya Maji kuhusu hatua zilizochukuliwa juu ya:

- i) kuthibitisha taarifa za uvujaji maji (NRW) ili kubainisha kama ziko sahihi kama zilivyowasilishwa na Mamlaka za Maji Mijini (UWSSAs), na
- ii) kufanya ufuatiliaji ili tathmini ni kwa kiwango gani mapendekezo yaliyotolewa kwa Mamlaka za Maji yametekelezwa.



Usimamizi wa Matengenezo ya Magari ya Serikali

Tulicho- chunguza

Wizara ya Ujenzi ina wajibu wa kusimamia magari ya serikali. Hii ni pamoja na manunuzi, usajili na matengenezo. Wakala wa Umeme na Matengezo (TEMESA) ana mamlaka na anawajibika kwenye matengenezo ya magari ya Serikali. Pia ana jukumu la kusimamia gereji binafsi zilizoidhishwa kutengeneza magari ya Serikali.

Ukaguzi ulichunguza kama:

- Wizara ya Ujenzi imeandaa mfumo endelevu kwa ajili ya usimamizi wa matengenezo ya magari ya serikali ikiwa ni pamoja na sera na taratibu kama chombo elekezi.
- matengenezo na ukarabati wa magari ya serikali hufanyika kwa tija na ufanisi kwa lengo la kuyaweka magari katika hali ya kufanya kazi vizuri na kupunguza matengenezo yasiyotarajiwa,
- TEMESA kama chombo kwa ajili ya kukarabati na kutengeneza magari yanayomilikiwa na serikali, inasimamia, inafuatilia na kutathmini utendaji wa gereji binafsi zilizoidhinishwa kutengeneza magari ya serikali, na
- Wizara ya ujenzi inasimamia vya kutosha na kutathmini utendaji wa TEMESA.

Wizara mbili zinazotumia magari ya Serikali ambazo ni Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, zilichaguliwa kwa lengo la kupima utendaji wa mfumo uliowekwa. Ukaguzi ulihusu matengenezo ya magari yaliyofanyika katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo kuanzia 2008/09 mpaka 2010/11.

Kwanini ni muhimu

Magari yanayomilikiwa na serikali yamekuwa yakiongezaka kwa idadi. Magari haya yanamilikiwa na vyombo vya serikali zaidi ya 200 (Serikali za Mitaa, Wizara na Idara za serikali) na Wizara ya Ujenzi ina wajibu wa kuhakikisha usalama wa magari hayo.

Kwa kuzingatia ukweli kwamba mfumo wa usimamizi wa magari ya serikali unakabiliwa na hatari kubwa, ufanisi katika usimamizi ni muhimu zaidi kulingana na ongezeko la magari ya Serikali. Kwa mfano, kati ya magari na pikipiki 65,252 zilizosajiliwa, hakuna kumbukumbu kamili inayoonesha ni magari yapi yanafanya kazi na ni yapi bado yanamilikiwa na serikali.

Tulicho-kiona

Wizara ya Ujenzi kama wizara husika katika usimamizi wa magari ya serikali haijaweka mfumo bora wa kusimamia matengenezo ya magari ya serikali. Aidha, hakuna sera ya matengenezo ya magari ya serikali. Hivyo, kuna upungufu wa miongozo juu ya usimamizi wa matengenezo ya magari ya serikali.

Hakuna viwango vya ubora na miongozo iliyoanzishwa kwa ajili ya kushughulikia matengenezo ya magari yanayomilikiwa na serikali. Pamoja na umuhimu wa matengenezo ya magari ya serikali, Wizara ya Ujenzi haijaanzisha utaratibu wowote ambao ungeweza kutumiwa na TEMESA na taasisi ambazo ndiyo watumiaji wa magari ya serikali kuhusiana na matengenezo ya magari ya serikali.

Wizara ya Ujenzi haifuatili vya kutosha utendaji wa shughuli za TEMESA. Wizara ya Ujenzi haijawahi kutathmini utendaji wa TEMESA wala taasisi za

serikali ili kubaini ni jinsi gani matengenezo ya magari yanayomilikiwa na serikali yanaboreshwa.

Pia ilibainika kuwa Wizara ya Ujenzi haina orodha ya karibuni ya magari ya serikali kama chombo cha kufuatilia matengenezo ya magari ya serikali.

Matengenezo ya magari yanayomilikiwa na serikali hayasimamiwi kwa ufanisi na TEMESA. Hii ni kwa sababu si magari yote yanayomilikiwa na serikali hufanyiwa ukaguzi kabla na baada ya matengenezo

Uteuzi wa gereji binafsi kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa magari yanayomilikiwa na serikali umekuwa ukichelewa kila mwaka na mara nyingi TEMESA imekuwa haihusishwi kwenye mchakato mzima.

Utendaji wa gereji na karakana binafsi haufuatiliwi kwa kiasi cha kutosha. TEMESA haina utaratibu wala mipango katika mpango wake wa kila mwaka, wa jinsi gani itafuatilia utendaji wa gereji binafsi. Ukosefu wa mipango ya ufuatiliaji katika mipango ya TEMESA ya kila mwaka, inaonesha kwamba TEMESA imejiengua kwenye wajibu wake wa kusimamia matengenezo ya magari yanayomilikiwa na serikali.

Ziara za kutembelea karakana za TEMESA zilizopo Dar-es-Salaam (yaani MT Depot na Vingunguti) zilibainisha kuwa karakana hizi zilikuwa na vifaa vingi chakavu ama havifanyi kazi. Vifaa muhimu kwa shughuli za karakana vipo kwenye hali mbaya.

TEMESA imekuwa ikitoa huduma ya matengenezo ya magari yanayomilikiwa na Taasisi na Idara mbalimbali za serikali. Hata hivyo taasisi hizo zimekuwa hazilipi na kufanya deni la matengenezo

kufikia Shilingi za Kitanzania Bilioni 3.9 hadi Desemba 2010.

Hitimisho

Wizara ya Ujenzi haijaweka mfumo sahihi wa kusimamia matengenezo ya magari ya serikali. Matengenezo ya magari yanayomilikiwa na serikali hayasimamiwi kwa ufanisi. Utendaji wa gereji na karakana binafsi haufuatiliwi vya kutosha.

Utendaji wa TEMESA haufuatiliwi vya kutosha na Wizara ya Ujenzi. Wizara ya Ujenzi haina mipango ya kufuatilia utendaji wa TEMESA juu ya suala la matengenezo ya magari ya serikali na tathmini haijawahi kufanyika katika eneo hili.

Masuala ya kuzungu- mza na Maafisa Masuuli

Muhtasari huu na taarifa kamili ya ukaguzi wa thamani ya fedha kuhusu matengenezo ya magari ya serikali unaweza kutumiwa na Kamati ya Hesabu za Serikali kuwauliza Maafisa Masuuli hatua walizochukua katika:

- i) Kuanzisha sera ya matengenezo ya magari ya serikali ambayo itatumiwa na taasisi zote za serikali.
- ii) Kuanzisha orodha mpya ya magari ya serikali, ambapo magari yote yanayomilikiwa na serikali yataorodheshwa na itatumika katika kupanga matengenezo ya magari hayo.
- iii) Kuhakikisha magari ya serikali yanakaguliwa kikamilifu kabla na baada ya matengenezo ili kuhakikisha ubora wa huduma.
- iv) kuanzisha mwongozo unaoshughulikia matengenezo ya magari ya serikali utakaotumiwa na mafundi katika gereji binafsi na zile za wakala.
- v) kufuatilia na kutathimini utendaji wa gereji binafsi zilizoidhinishwa kutengeneza magari ya serikali.

- vi) kuimarisha mawasiliano kati ya taasisi za serikali zinazosimamia na kutumia magari ya serikali.
- vii) kutoa miongozo mara kwa mara ambayo itasambazwa kwenye taasisi za serikali juu ya usimamizi wa matengenezo ya magari ya serikali.
- viii) kuimarisha karakana za TEMESA ziweze kufikia mahitaji ya viwango vya matengenezo.
- ix) kuhamasisha taasisi za serikali kulipa gharama za huduma za matengezo ya magari zilizotolewa na TEMESA kwa wakati ili kurahisisha utendaji kazi wa TEMESA.



Tulichochunguza

Isimamizi wa uvunaji wa misitu

engo kuu la Wizara ya Maliasili na Utalii ni kutunga sera na kuweka mikakati ya usimamizi endelevu na uhifadhi wa maliasili za nchi ili kuongeza mchango wa sekta katika mapato yanayokusanywa na serikali. Idara ya Misitu na Nyuki inawajibu wa kuandaa sera na sheria. Kupitia Idara ya Misitu na Nyuki, Wizara inatakiwa kujenga uwezo, kuwezesha, kufuatilia na kutathmini shuguli za misitu katika ngazi ya Mkoa na Wilaya.

Kwa sasa, baadhi ya majukumu ya Idara ya Misitu na Nyuki yamechukuliwa na Wakala wa Huduma ya Misitu kama shirika lisilokuwa na uhuru kamili wa kujiamulia mambo yake na linalojiendesha kifedha. Wakala wa Huduma ya Misitu ina wajibu wa kusimamia uhifadhi wa misitu na rasilimali zitokanazo na nyuki ili kuhakikisha kuna uzalishaji endelevu wa bidhaa hizi.

Tulichunguza ufanisi wa mifumo ya udhibiti uliowekwa na Wizara ili kuhakikisha kuwa mapato yanayotokana na uvunaji misitu yanakusanywa kikamilifu. Pia tumetathmini utendaji wa vizuia na vikosi vya doria za misitu katika kukabiliana na uvunaji na biashara haramu za misitu.

Ukaguzi umelenga uvunaji wa misitu inayomilikiwa na serikali kuu. Halmashauri za Wilaya sita zenye uvunaji mkubwa wa miti zilichaguliwa kwa ajili ya uchunguzi. Ukaguzi uliendana sambamba na taarifa za fedha za mwaka 2008-2011.

Kwanini ni muhimu

Tanzania Bara ina eneo la misitu lipatalo hekta 33,4 milioni (FAO 2010)¹. Rasilimali hii inakabiliwa na shinikizo kubwa la uvunaji holela. Kwa mujibu wa FAO (2010), wastani wa kiwango cha ukataji miti kati ya mwaka 1990 na 2010 ni hekta 403,000 kwa mwaka. Hasara hii kwa misitu ya Tanzania inachochewa na kasi ya kilimo cha kuhama hama, maendeleo ya makazi, uchimbaji barabara na madini, ufugaji wa kupita kiasi, moto usiodhibitiwa na ukataji miti kwa ajili ya mkaa na mbao. Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na tatizo kubwa la uvunaji haramu wa miti ambao umeinyima mapato serikali na imekuwa tatizo kubwa Tanzania.

Katika tukio moja, zaidi ya makontena 100 yenye mbao zilizopatikana kinyume cha sheria zilikamatwa katika bandari ya Dar es Salaam mwaka 2004. Magogo ya aina ya miti ambayo hayaruhusiwi kusafirishwa nje yalikutwa katika makontena hayo. Desemba 2009, Wizara ya Maliasili na Utalii imeripoti kuwa 57% ya mapato (wastani wa shilingi za kitanzania bilioni 23) kutoka na mazao ya misitu hayakukusanywa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009.

Baadhi ya sababu zilizoripotiwa kuhusiana na mapato yasiyokusanywa ni pamoja na ukwepaji wa malipo ya kodi, udanganyifu (ikiwa ni pamoja na kughushi nyaraka za mapato). Kwa sababu ya matatizo haya kumekuwa na mijadala katika bunge, miongoni mwa wataalam wa misitu na umma juu ya haja ya kuboresha udhibiti katika biashara ya uvunaji na usafirishaji wa mazao ya misitu Tanzania.

¹ Ripoti ya Shirika la Chakula 2010

Tulicho -kiona

Wizara ya Maliasili na Utalii haijaweka udhibiti wa kutosha wa kuhakikisha kuwa mapato yatokanayo na uvunaji wa misitu yanakusanywa ipasavyo.

Nchini Tanzania, asilimia nne (4%) tu (35) ya misitu ina Mipango ya Usimamizi wa Misitu na ilyobaki 96% inafanya kazi bila kuwa na mipango.

Wizara haina utaratibu mzuri wa kudhibiti utoaji wa leseni katika ngazi ya wilaya kwani ilibainika baadhi ya wilaya zimetoa leseni za uvunaji, vibali vya usafirishaji mazao ya misitu bila kuwa na Mipango ya Usimamizi wa Misitu na ile ya uvunaji ya mwaka.

Kamati za Uvunaji Misitu za Wilaya hazitoi taarifa kwa Wizara ya Maliasili na Utalii maamuzi yaliyofikiwa katika mikutano yao ya kujadili maombi ya uvunaji. Hii inakosesha Wizara taarifa muhimu kama vile idadi ya watu walipewa leseni katika kila mkutano na kiasi cha miti kilichopitishwa kwa uvunaji. Hii inapelekea Wizara kutokuwa na uwezo wa kutathmini ni kwa kiasi gani malengo ya Kamati za Uvunaji Misitu za Wilaya yanafanikiwa.

Katika wilaya sita zilizotembelewa, ilibainika kuwa kuna uhaba wa wafanyakazi. Hii ilipelekea Maafisa Misitu wa Wilaya kufanya kazi mbalimbali na kusababisha kuelemewa na mzigo wa kazi. Ni jambo la kawaida kuona ofisi hiyo yenye jukumu la utoaji wa leseni, ukusanyaji wa mapato, uwekajialama ya nyundo kwa miti iliyovunwa, kufanya doria na kuhudhuria masuala mengine ya kiutawala ambayo si ya kitaalam katika usimamizi wa misitu .

Mwongozo wa uvunaji endelevu wa misitu haufatiliwi kikamilifu. Kamati za Uvunaji Misitu za Wilaya hazifanyi mikutano kila baada ya miezi mitatu

kujadili mwelekeo wa shuguli za uvunaji kama inavyotakiwa na miongozo. Katika baadhi ya Wilaya zenye uvunaji mkubwa, Kamati ya Uvunaji haikufanya vikao kabisa katika mwaka wa 2010. Kwa sababu hii, watu ambao walihitaji vibali vya kuvuna hawakuweza kupewa na hii imechangia uvunaji wa misitu kinyume cha sheria.

Maofisa kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii makao makuu hawafanyi ufuatiliaji wa mara kwa mara wa shughuli za uvunaji wa misitu kwa kutembelea wilaya zenye misitu inayovunwa. Matokeo yake, wizara haijui hali halisi ya maeneo uvunaji unakofanyika.

Afisa Misitu wa Wilaya mara chache hutembelea maeneo ya uvunaji na wengi wao hawakagui yale maeneo magogo yalikovunwa kama inavyotakiwa na sheria na muongozo wa uvunaji. Mara nyingi, magogo hugongwa nyundo baada ya kutolewa eneo la uvunaji au wakati mwingine yanapelekwa katika ofisi ya Afisa Misitu wa Wilaya.

Wizara haijaweza kubainisha kupanda au kushuka kwa utendaji wa vizuizi na vikosi vya doria. Hii ni kwa sababu wizara mara kwa mara haipitii wala kuchambua kiufanisi taarifa za vizuizi na vikosi vya doria ili kujua utendaji wake.

Faini na adhabu zilizoainishwa na kutekelezwa kwa wafanyabiashara haramu waliokamatwa na mazao ya misitu ni za chini sana. Faini ya kiwango cha chini haiwezi kumuumiza mvunaji haramu ili kuachana na biashara haramu ya mazao ya misitu.

Hakuna Mkataba wowote wa makubaliano ya utendaji kazi uliosaniwa kati ya TAMISEMI na Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu usimamizi wa uvunaji wa

misitu katika Wilaya. Ilibainika kwamba mamlaka zote mbili zina malengo yanayopingana juu ya usimamizi wa misitu.

Utaratibu wa uwajibikaji wa vikosi vya doria na vizuia katika kupambana na uvunaji haramu wa magogo sio sahihi. Kuna matukio ya mgongano wa maslahi unaosababishwa na vitengo viwili kuwajibika kwa Mkurugenzi msaidizi matumizi (Assistant Director of Utilization).

Hakuna vizuia vya Wizara ya Maliasili na Utalii katika maeneo yenye uvunaji mkubwa kama vile Morogoro, Kigoma na Mbeya. Ilifahamika kuwa kati ya vizuizi 26 vilivyojengwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, 16 (zaidi ya 60%) viko katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Mgawanyo wa rasilimali (fedha, watu na vifaa) kwa vikosi vya doria haufanyiki ipasavyo. Wizara inagawanya rasilimali kwa njia ya majadiliano na makubaliano kwa kuangalia mahitaji ya wakati husika. Wizara ya Maliasili na Utalii haina vigezo na fomula maalumu inayotumika kwa ajili ya kugawa fedha, watumishi na vifaa vya kufanyia kazi katika vikosi vya doria.

Mfumo wa kukusanyia Taarifa (NAFOBEDA) hauna taarifa zinazoendana na wakati ili kuwawezesha Wizara ya Maliasili na Utalii kuboresha misitu nchini.

Kwa ujumla, udhibiti uliowekwa na wizara kuhakikisha mapato yatokanayo na uvunaji misitu yanakusanywa kikamilifu haufanyi kazi vizuri. Pia wizara haijaweka nguvu kubwa kusaidia na kufuatilia utendaji wa vizuia na vikosi vya doria katika kushughulikia tatizo la uvunaji na biashara haramu ya mzao ya misitu.

itimisho

Udhaifu wote huu unaizuia serikali kupata mapato na pia kutekeleza mbinu endelevu ya usimamizi wa misitu.

**Masuala
ya
kuzungu-
mza na
Afisa
masuuli**

Muhtasari huu na ripoti kamili ya ukaguzi wa ufanisi inaweza kutumiwa Kamati Hesabu za Serikali au kamati za kisekta zinazohusika na usimamizi wa misitu katika kuibua maswali kwa Maafisa Masuuli juu ya hatua za kuchukuliwa ili kuhakikisha kwamba:

- i. Uvunaji unazingatia Mipango ya Usimamizi ya Misitu iliyoidhinishwa.
- ii. Kunakuwepo utaratibu wa kutathmini ubora wa Mipango ya Usimamizi iliyotayarishwa na Afisa Misitu wa Wilaya na utekelezaji wake.
- iii. Mfumo wa ufuatiliaji wa mapato yanayokusanywa kutoka kwenye miti inayovunwa inarandana na kiasi cha ujazo kinachovunwa, aina ya mti na kiwango sahihi cha mrahaba kinachotozwa.
- iv. Fomula ya kukokotoa kiasi cha mrabaha kitakacholipwa inazingatia mambo muhimu kama vile bei ya soko, gharama ya nafasi na mambo mengine na kufuatiliwa ipasavyo.
- v. Utaratibu wa uvunaji bidhaa za misitu unafuatwa kama ilivyoagizwa na miongozo ya uvunaji wa misitu.
- vi. Shughuli za vizuia na vikosi vya doria zinawekewa mipango mizuri kwa kuzingatia vihatarishi na utendaji wao utathiminiwe kwa ufanisi.
- vii. Rasilimali watu, vifaa, na kujenga uwezo kwa watumishi wa vizua na vikosi vya doria

vinazingatiwa ili kuboresha utendaji wao.

- viii. Vizuia viwekwe kimkakati hasa kwenye maeneo yenye uvunaji mkubwa ili kuweza kupamabana na uvunaji haramu.
- ix. Viwango vya faini na adhabu vinavyotolewa vinakuwa na athari zinazokusudiwa ili kuzuia makosa uvunaji haramu yasitendeke
- x. Kunakuwepo mfumo mzuri wa mawasiliano wenye ufanisi na vyombo vya kutekeleza sheria.



Tulichochunguza

Usimamizi wa mapato yanayokusanywa na wakala

Wakurugenzi wa halmashauri wana wajibu wa kukusanya mapato ya halmashauri. Wao ndiyo wanafanya maamuzi juu ya kutumia mawakala binafsi katika kazi ya ukusanyaji wa mapato. Pia wana wajibu wa kuhakikisha kuwa kuna usimamizi madhubuti wa mikataba wanayoingia na mawakala binafsi kwa ajili ya kukusanya mapato. Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI) ina jukumu la kusimamia fedha za serikali za mitaa ikiwa ni pamoja na utoaji wa msaada wa kiufundi, kuzijengea uwezo halmashauri na kufuatilia ukusanyaji wa mapato katika halmashauri (hupokea taarifa za utekelezaji za kila robo mwaka kwa kupitia Katibu Tawala wa Mkoa (RAS), kufanya ukaguzi wa mara kwa mara, wa kushtukiza na wa bajeti za serikali za mitaa).

Ukaguzi ulichunguza kama kazi ya kukusanya mapato kwa kutumia wakala binafsi ilisimamiwa na mamlaka ya serikali za mitaa kwa ufanisi na kikamilifu na kama taratibu hizi zilifuatiliwa na kutathminiwa ipasavyo na mamlaka za juu.

Ukaguzi huu ulilenga hasa kuangalia jinsi mamlaka za serikali za mitaa zinavyojiandaa kabla ya kufanya uamuzi wa kumpa wakala kazi ya kukusanya mapato; taratibu zinazotumika kumpata wakala wa kukusanya mapato; usimamizi wa mikataba; adhabu zilizopo pamoja na utekelezaji wa adhabu hizo. Hii ni pamoja na kuangalia ufuatiliaji na tathmini inayofanywa na Serikali Kuu yaani OWM-TAMISEMI na Wizara ya Fedha.

Ukaguzi uliangalia kipindi cha miaka 3 ya fedha yaani 2007/2008 mpaka 2009/2010. Vyanzo mbalimbali vya mapato vilichaguliwa kwa ajili ya uchunguzi katika halmashauri 14 za serikali za mitaa ambazo ni 11% ya Halmashauri zote 133 za Tanzania Bara. Hii ilichukuliwa kama sampuli toshelezi kwa ajili ya zoezi hili.

**Kwanini
ni
muhimu**

Halmashauri nyingi za Serikali za Mitaa nchini zimefanya marekebisho ya mfumo wa ukusanyaji wa mapato. Marekebisho hayo yalikusisha hasa kuwapa wakala binafsi kazi ya kukusanya mapato ya ndani ya Halmashauri. Hii inatoa fursa kwa halmashauri kuweza kuongeza mapato na kupunguza gharama.

Mpaka mwaka 2000, serikali nyingi za mitaa Tanzania Bara zilikuwa zinatumia sekta binafsi kukusanya mapato kwa niaba ya halmashauri hizo. Moja ya sababu za kukusanya mapato kwa kutumia wakala ilikuwa ni kuongeza tija katika ukusanyaji wa mapato na kupunguza gharama za kuratibu ukusanyaji ambazo zilikuwa zinalipwa na halmashauri.

Kazi ya kukusanya mapato ya halmashauri kwa kutumia wakala ni moja ya jitihada za sera mpya ya ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi (PPP) nchini. Lengo kuu la sera hii ni kutoa huduma bora kwa jamii kupitia ushirikiano wa pamoja wa sekta binafsi, serikali na wadau wengine..

Mapato ya serikali za mitaa ni muhimu kwa rasilimali za umma zinazotumika katika ngazi ya mtaa. Jinsi mapato mengi zaidi yatakavyokusanywa katika ngazi ya mtaa ndivyo bidhaa na huduma nyingi zaidi zitatolewa kwa jamii. Asilimia ya mchango wa mapato ya halmashauri yatokanayo na vyanzo vya

ndani kwa mapato yote ya Halmashauri katika ukusanyaji ni kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapa chini:

Mapato ya vyanzo vya ndani vya halmashauri yaliyokusanywa kama asilimia ya mapato yote ya halmashauri

	2005/6	2006/7	2007/8	2008/9	2009/10
Vyanzo vya ndani	7.2%	8.5%	9.2%	8%	7.5%
Vyanzo vingine ²	92.8%	91.5%	90.8%	92%	92.5%
Jumla	100%	100%	100%	100%	100%

Chanzo: Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali

Jedwali hapo juu linaonesha kwamba asilimia ya mapato ya halmashauri yanayotokana na vyanzo vya ndani ikilinganishwa na mapato yote ya halmashauri, ipo chini. Chanzo kikubwa cha mapato ni ruzuku kutoka serikalini. Ili serikali za mitaa ziweze kuongeza ukusanyaji wa mapato na kuwa endelevu, vyanzo vya ndani vya mapato lazima visimamiwe ipasavyo. Kulingana na mabadiliko katika serikali za mitaa, ushiriki wa sekta binafsi katika ukusanyaji wa mapato yao - ingawa si wa uhakika - unadhaniwa kuwa njia mojawapo ya kuongeza ukusanyaji wa mapato ya serikali za mitaa.

**Tulicho
-kiona**

Halmashauri hazifanyi kwa ufanisi uchunguzi wa soko la uwakala wa kukusanya mapato. Hakuna ushahidi wa kutosheleza kuonesha kwamba halmashauri zilifanya tathmini ya upatikanaji wa mawakala wenye uwezo wa kuchukua majukumu yao. Pia, majukumu mapya ya msimamizi wa mikataba

kuhusiana na mawakala wa kukusanya mapato hayakuwekwa bayana na uongozi wa halmashauri.

Taratibu zilizotumika kupata mawakala wa kukusanya mapato hazikufanyika kwa ufanisi. Hii ilisababishwa na ushindani mdogo kati ya wazabuni na pia ukosefu wa uwazi wa vigezo kwaajili ya tathmini ya zabuni. Karibu nusu ya zabuni zilibandikwa tu kwenye mbao za matangazo za halmashauri na hivyo kupunguza ushindani unakosudiwa katika uitishaji zabuni.

Mikataba hailindi maslahi ya halmashauri. Mikataba imeweka viwango visivyobadilika ambavyo mawakala wanatakiwa kupeleka kwa Halmashauri husika kila mwezi badala ya asilimia fulani ya kiasi chote kilichokusanywa. Hivyo, Mkurugenzi wa halmashauri hawezi kuwashtaki mawakala wa kukusanya mapato kwa kutopeleka kiasi chochote ambacho ni ziada ya kile walichokubaliana wakati ukusanyaji unapokuwa zaidi kuliko ilivyotarajiwa.

Utendaji wa mawakala wa kukusanya mapato haufuatiliwi kwa ufanisi. Hii ni kwa sababu ya kutokuwepo kwa ripoti za utendaji zinazowasilishwa na wakala kwa halmashauri.

Hakuna usuluisho (reconciliation) wa mara kwa mara uliofanywa na halmashauri kati ya vitabu vya stakabadhi vilivyotumiwa na mawakala wa kukusanya mapato dhidi ya kiasi kilichopelekwa halmashauri. Uwasilishaji wa taarifa za utendaji wa mawakala kwa halmashauri halikuwa sharti lililowekwa bayana kwenye mikataba iliyosainiwa kati ya halmashauri na mawakala wa kukusanya mapato.

Adhabu zilisimamiwa na kutekelezwa kwa nadra ingawa zilielezwa wazi katika baadhi ya sheria ndogo

na mikataba kati ya Halmashauri na mawakala wa kukusanya mapato. Pia, hakuna adhabu zilizotolewa kwa mawakala ambao aidha walipeleka mapato pungufu ya kiasi walichokubaliana kwenye mikataba ama walichelewa kupeleka makusanyo.

Kaguzi za ndani hazikushughulikia kwa kiasi cha kutosha changamoto za ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mawakala. Taarifa chache zimegusia kazi ya kukusanya mapato kwa kutumia wakala. Wakaguzi wa ndani mara chache walitoa taarifa juu ya matatizo ya ukusanyaji wa mapato yanayowakabili mawakala.

Hakuna tathmini ya kina iliyofanywa na kitengo cha fedha katika idara ya usimamizi wa huduma ya serikali za mitaa na OWM - TAMISEMI juu ya taarifa za maendeleo zilizowasilishwa na Halmashauri kila robo mwaka. Kitengo cha fedha kiliandaa na kuchambua tu taarifa moja moja na ya jumla ambazo zilionyesha bajeti dhidi ya makusanyo halisi.

Halmashauri hazina mipango madhubuti kabla ya kubinafsisha ukusanyaji wa mapato kwa wakala binafsi. Taratibu zinazotumika kutafuta mawakala wa kukusanya mapato hazitekelezwi ipasavyo. Mikataba haiandaliwi vizuri kulinda maslahi ya halmashauri. Utekelezaji wa mikataba na utendaji wa mawakala hausimamiwi kwa ufanisi na halmashauri.

Tathmini na ufuatiliaji wa mara kwa mara uliofanywa na mamlaka za juu OWM-TAMISEMI/Wizara ya Fedha hauna ufanisi.

**Masuala
ya
kuzungu-
mza na
Afisa
Masuuli**

Muhtasari huu wa ripoti pamoja na ripoti kamili ya ukaguzi wa ufanisi juu ya usimamizi wa kazi ya ukusanyaji wa mapato inayotolewa na Halmashauri

kwa wakala inaweza kutumiwa na Kamati ya Hesabu za Serikali kuwahoji Maafisa Masuuli juu ya hatua zilizochukuliwa kuhakikisha kwamba:

- Kuna ufanisi katika mfumo wa kufuatilia na kutathmini utendaji wa halmashauri katika shughuli za kukusanya mapato
- Uamuzi wa kuwapa wakala kazi ya kukusanya mapato ya ndani ya halmashauri unalinda maslahi ya halmashauri husika
- Mantiki ya kukusanya mapato kwa kutumia wakala ithibitishwe kabla hijaanza kutekelezwa
- Mikataba kati ya halmashauri na wakusanya mapato inafanyiwa kazi kwa usahihi na kadiri inavyowezekana inapaswa kulinda maslahi ya halmashauri
- Mifumo ya kudhibiti na kutathmini imewekwa ili kusimamia utendaji wa mawakala wa kukusanya mapato



Utangulizi

Madhumuni ya Ukaguzi

Sura ya 3

Ukaguzi wa Kiuchu- nguzi

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilianza kufanya ukaguzi wa kiuchunguzi tangu mwishoni mwa mwaka 2007 kwa madhumuni ya kukuza nidhamu katika matumizi ya fedha na kudhibiti vitendo vya ubadhirifu katika shughuli za serikali.

Kujenga imani kwa jamii katika maamuzi yatokanayo na ukaguzi ni muhimu ili kukubalika kwa kazi ya ukaguzi; pia inachangia katika kuaminika kwa hesabu za taasisi zilizokaguliwa. Ukaguzi wa kiuchunguzi unaweza kutumika kurejesha imani ya jamii na ile ya wafadhili wa ndani na nje juu ya matumizi ya rasilimali za umma katika taasisi mbalimbali.

Mamlaka

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu anayo mamlaka ya kufanya ukaguzi wa kiuchunguzi chini ya Kifungu cha 27 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya 2008. Kanuni Na.83 ya ukaguzi wa Umma 2009 inamtaka kuagiza kufanyika ukaguzi wa kiuchunguzi mara apatapo taarifa ya tuhuma za udanganyifu kupitia afisa wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, na baada ya kujiridhisha kwamba inawezekana udanganyifu unaotiliwa shaka kuwa umetokea ndani ya taasisi yoyote anayoikagua.

Vilevile Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kufanya ukaguzi maalum. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu anapaswa kuandaa taarifa ya ukaguzi maalum kuhusiana na masuala yaliyochunguzwa na kisha kuiwasilisha taarifa husika kwa Mhe.Rais.

Viwango vya Ukaguzi

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania (NAOT) ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi za Nchi (INTOSAI), Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi kwa Mataifa yya Afrika (AFROSAI), na lile la Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi kwa Nchi za Afrika zinazozungumza Kiingereza (AFROSAI-E). Kama mwanachama wa mashirika haya ya kimataifa, NAOT inapaswa kuzingatia mahitaji ya viwango vya ukaguzi vya INTOSAI, na viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi za Kitaifa ISSAIs. Viwango hivi vinahitaji kuwa timu ya ukaguzi ipange na kutekeleza ukaguzi ili kupata ushahidi sahihi na wa kutosha kwa ajili ya kuweka misingi ya matokeo ya ukaguzi na kufanyika maamuzi kulingana na malengo ya ukaguzi. Timu ya ukaguzi inaamini kuwa ushahidi uliopatikana unatoa msingi stahili wa matokeo ya ukaguzi na hatima iliyozingatia malengo ya ukaguzi.

Lengo la Taarifa hii ya Jumla

Lengo la taarifa hii ya jumla ya ukaguzi wa kiuchunguzi ni kuweza kuwafahamisha Wahe. wabunge, serikali na wadau wengine juu ya matokeo ya kaguzi za kiuchunguzi zilizofanyika hadi sasa. Taarifa zinaweza kutumika kwa ajili ya kuwahoji Maafisa Masuuli kuhusu hatua zilizochukuliwa kukabiliana na vitendo vya udanganyifu vinavyoweza kutokea ili kuzuia udanganyifu kama huo kwa siku zijazo.

Mchakato wa uthibitishaji/uhakiki wa taarifa

Mamlaka zilizokaguliwa za Mfuko (NHIF) na ya Halmashauri ya Wilaya (Misungwi) zilipewa fursa ya kujadili na kutoa maoni yao juu ya matokeo ya ukaguzi ili kupata usahihi na kudhibiti makosa katika taarifa husika.

Muundo wa taarifa

Sura hii ina muhtasari wa taarifa mbili za ukaguzi wa kiuchunguzi kuhusiana na mambo yaliyochunguzwa, umuhimu wake, yaliyobainika, hitimisho na masuala muhimu kwa Maafisa Masuuli. Taarifa hizo ni ile ya Usimamizi wa bili toka kwa watoa huduma ya afya kwenda Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, na ya ukaguzi Maalum wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi.



Usimamizi juu ya madai ya watoa huduma ya Afya kwa Mfuko wa Bima ya Afya

Tulichochunguza

Kama sehemu ya mpango wa mageuzi katika Sekta ya Afya, mnamo mwaka 1993 Serikali ilianzisha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya chini ya Sheria ya Bima ya Afya Na.8 ya mwaka 1999. Lengo kuu lilikuwa ni kutoa huduma za afya kwa wafanyakazi katika sekta rasmi. Hadi sasa Bima ya Afya imesajili watoa huduma 526 wenye ngazi tofauti za vifaa na utaalamu; ambao ni hospitali binafsi na zile za Serikali kwa ajili ya kutoa huduma za afya kwa wanachama wa Bima ya Afya ambapo madai yao hulipwa baadae na Mfuko.

Tulichunguza iwapo kulikuwa na vitendo vya udanganyifu wakati wa mchakato wa maandalizi, ushughulikiaji na ulipaji madai yaletwayo na watoa huduma kwa Mfuko pamoja na malipo yaliyofanyika. Ukaguzi ulifanya yafuatayo:

- tulichunguza ufanisi katika udhibiti uliowekwa katika kuzuia, kubaini na kusahihisha vitendo vya ubadhirifu/udanganyifu
- tulihakiki uhalali wa taarifa za wagonjwa zilizotumika kwa ajili ya malipo
- tulihakiki uhalali wa malipo na uhalisia wake.
- tuliainisha aina ya udanganyifu na hasara iliyosababishwa, na
- tuliainisha kiwango cha hasara iliyopatikana katika thamani ya fedha

Wigo wa ukaguzi ulijikita katika kuhakiki nyaraka, kufanya mahojiano, na kubaini kwa kushuhudia namna ambavyo huduma ilitolewa. Hasa

tulichunguza nyaraka zifuatazo: rejista za kusajili wagonjwa walioingia na kutoka hospitali, daftari za kumbukumbu za maabara na duka la madawa; fomu za madai 2A&B, na 2C; ripoti za madai ya mwezi na majalada ya wagonjwa pamoja fomu zilizotolewa na daktari kutoa maagizo ya dawa.

Tuliwakagua watoa huduma wakubwa na wadogo ambao ni “Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Kilimanjaro Christian Medical Centre (KCMC), Vituo vya Afya vya Faraja (FHC) na Moshi Upendo (MUHC)”

**Kwanini
ni
muhimu**

Mfuko wa Bima ya Afya hugharamia huduma za afya kupitia watoa huduma za afya waliosajiliwa na Mfuko. Mfuko wa Bima ya Afya husajili na kutoa huduma za afya kwa wanachama wake wanaoongezeka kwa idadi na walioenea nchi nzima. Wanachama wa Bima ya afya wamegawanyika katika madaraja mawili ya walio na kadi za kijani na wale wenye kadi za kahawia. Vivyo hivyo, watoa huduma wamegawanyika katika makundi mbalimbali kulingana na uwezo wa kitaalamu, na miundo mbinu na vifaa walivyonyavyo. Hali iliyopo haitoi uhakika wa ufanisi kwa udhhibiti wa ndani wa madai yaliyotokana na huduma za afya kwa watoa huduma kwenda kwenye Mfuko.

Hata hivyo, kulikuwa na malalamiko kutoka kwenye jamii kuhusu huduma zinazogharamiwa na Bima ya afya kupitia kwa watoa huduma. Mfuko wa Bima ya Afya ulilalamikia ukiukwaji wa mwenendo wa utoaji huduma za afya kwa baadhi ya watoa huduma kupitia vyombo vya habari. Vivyo hivyo, kulikuwa na malalamiko kwamba baadhi ya wanachama wa Mfuko walinyimwa kupata huduma za afya na pengine kutakiwa kulipia huduma hizo katika baadhi vituo vya watoa huduma.

Tulichokiona

Ufuatao ni muhtasari wa matokeo ya ukaguzi wa kiuchunguzi:

Wanachama Batili waliopatiwa huduma za NHIF

Uhakiki uliofanyika katika baadhi ya kumbukumbu za wagonjwa zilizopatikana katika Hospitali ya Muhimbili kwa kipindi kilichoanzia Novemba 2009 hadi Oktoba 2010, na kulinganishwa na kumbukumbu za wanachama katika taarifa za wagonjwa zilizopatikana katika 'database' ya Mfumo Funganifu wa Kumbukumbu za Wanachama (MMIS) ulibaini idadi ya wagonjwa batili 7053 waliofika hospitalini mara 26,725 kwa ujumla wake.

Hali hii ilithibitika kutokana na ukweli kwamba taarifa kutoka katika Mfumo Funganifu wa Kumbukumbu za Wanachama 'MMIS' hazikuendana na taarifa zilizopatikana katika Hospitali ya Muhimbili. Huduma zilizotolewa kwa watu hao ziliugharimu Mfuko kiasi cha Sh.503,920,000 ikiwa ni malipo kwa kipindi chote.

Udhibiti usiokidhi katika uwekaji wa kumbukumbu na utoaji huduma ya vipimo vya Kiaguzi

Uhakiki wa madai kwa kipindi cha Novemba 2009 kwa KCMC, Machi 28 hadi Aprili 30 kwa MUHC na Julai 2008 kwa FHC na rejista kwa ajili ya vipimo mbalimbali vya kiaguzi yalibaini kuwa baadhi ya vipimo havikuthibitika kufanyika. Hii ni kinyume na Kifungu cha 27 cha Sheria ya Bima ya Afya ya mwaka 1999 ambacho kinahitaji kuhakikisha unakuwepo ufuatiliaji katika utaratibu wa ndani wa vituo vya watoa huduma ili kudhibiti taratibu za kiaguzi zisizofaa.

Malipo maradufu yaliyofanyika kutokana na huduma za afya zilizotolewa KCMC

Fomu za madai za mwezi Julai 2008 zilizohakikiwa pamoja na mafaili husika ya wagonjwa zilionesha uwepo wa wagonjwa watano ambao walilipia gharama zao za huduma ya malazi wao wenyewe. Hata hivyo gharama hizo zilitozwa pia katika madai yaliyoelekezwa kwa Mfuko, hivyo kuwa yametoza mara mbili na kulipwa.

Taarifa zisizojitosheleza za madai ya gharama za Dawa zilizotozwa na KCMC

Dawa zilizotolewa kwa wagonjwa kupitia chumba cha kutolea dawa (General Pharmacy) katika hospitali ya KCMC zilibainika kuwa na mashaka. Kumbukumbu zilizo katika mafaili ya wagonjwa hazikuonesha kuwa dawa zilizotolewa ziliandikwa na madaktari kwa wagonjwa husika. Hata hivyo, madaktari wanapaswa kuandika maelekezo ya dawa zitolewazo kwa wagonjwa kwenye majalada yao ili kudhibiti na kurahisisha ufuatiliaji.

Ufanisi usiokidhi katika Udhibiti wa Mfumo Funganifu

Data zilizomo katika mfumo ulioanzishwa (MMIS) zilibainika kutoamika kulingana na uhakiki uliofanywa katika taarifa na maswali ya kimfumo (system inquiries) kuhusiana na utambuzi wa wanachama ndani ya mfumo. Ilibainika kuwa mfumo huo funganifu 'MMIS' haukuwezesha kubaini matumizi ya namba za utambulisho wa uanachama yaliyoingiliana, ambapo katika hali ya kawaida mfumo ulipaswa kubaini na kukanusha taarifa yoyote isiyo sahihi itakayotaribu kuingizwa.

Kwa kuzingatia mambo yaliyobainika kwenye ukaguzi huu wa kiuchunguzi uliofanyika tunahitimisha kwamba:

- Mfuko wa Bima ya Afya una udhaifu katika udhibiti wa madai yanayotolewa na watoa huduma yahasuyo vipimo vya kiaguzi
- utaratibu katika udhibiti wa utoaji wa dawa umedhihirika kuwa na udhaifu
- Mfumo Funganifu ulioanzishwa "MMIS" haufanyi kazi kwa ufanisi. Mfumo huo una baadhi ya taarifa zisizo sahihi hali iliyosababishwa na kukosekana kwa utaratibu madhubuti wa usimamizi wa 'database'.

**Masuala
ya
kuzungu-
mza na
Afisa
Masuuli**

Ripoti hii ya jumla pamoja na ripoti yake kamili ya Ukaguzi wa Kiuchunguzi wa madai ya watoa huduma za afya kwenda Bima ya Afya zinapaswa kutumiwa na Bodi ya Wakurugenzi pamoja na Menejimenti ya Mfuko katika kuboresha hali iliyobainika kwa kusahihisha udhaifu uliobainika katika mfumo wa madai ya watoa huduma kuhakikisha kuwa:

- (i) watoa huduma wote wanatakiwa kuweka utaratibu madhubuti wa kuhakikisha kwamba taarifa zinazohusu madai ni za kweli na sahihi,
- (ii) kuhakikisha uimarishwaji wa mfumo wa usimamizi wa 'database' ili kuleta usahihi na uhakika wa taarifa, na
- (iii) kuweka utaratibu wa ufuatiliaji juu ya utendaji kazi wa watoa huduma.



Ukaguzi Maalum Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi

Tulichochunguza

Mkurugenzi wa Halmashauri ana wajibu wa kuhakikisha uwepo wa mfumo wa usimamizi wa fedha ulio rasmi na wa kuridhisha katika Halmashauri. Hii ni pamoja na mipango sahihi kwa ajili ya wafanyakazi na usimamizi wa idara ya fedha. Pia ana majukumu ya usimamizi wa jumla wa matumizi yote ya Halmashauri na mapato; pamoja na mali na madeni yake.

Tulichunguza mapato na matumizi ya Halmashauri katika maeneo yafuatayo: uuzwaji wa mali za Halmashauri, mishahara, madeni kwa akaunti za Benki (Overdrafts), miradi ya maji na kilimo, Ujenzi wa matenki ya maji, ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi, Majengo ya Halmashauri, Masurufu yasiyorejeshwa na mahusiano ya Kiutendaji baina ya viongozi na watendaji wa Halmashauri.

Ukaguzi ulilenga mwaka wa fedha 2008/09 na 2009/10.

Kwa nini ni Muhimu

Taarifa za ukaguzi za Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu zilizopita zimeonesha masuala mbalimbali makubwa yanayohusu upungufu wa udhibiti wa ndani katika Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi. Vile vile, kumekuwa na malalamiko mbalimbali yanayohusiana na migogoro kati ya wafanyakazi na madiwani ambapo mapendekezo yalitolewa yalibakia bila kutatuliwa.

Ilikuwa ni muhimu kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu kufanya ukaguzi huu maalum kama ilivyoainishwa chini ya Kifungu Na. 36 cha Sheria ya Ukaguzi wa

**Tulicho-
kiona**

Umma ya mwaka 2008, ambacho kinasema kuwa 'wakati wowote Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Seikali akiona inahitajika atalijulisha Bunge kwa suala lolote bila kuchelewa kuhusiana na fedha au mali ya umma, ataandaa ripoti maalumu kuhusiana na suala hilo.

Malipo Hewa Yenye Jumla ya Sh.43,668,000

Kiasi cha jumla ya Sh. 43,668,000 kilithibitika kutumika kwa ajili ya manunuzi hewa ya shajala kwa matumizi ya vijiji 78 na kata 20.

Mishahara Isiyolipwa isiyorejeshwa Hazina Sh. 24,581,698

Mishahara isiyolipwa tangu Agosti 2008 hadi Julai 2010 kiasi cha Sh.24,581,698.80 haikurejeshwa hazina kupitia Katibu Tawala Mwanza. Halmashauri iliandaa hundi Na.07688 ya tarehe 4/1/2011 ya kiasi cha Sh.23,932,205 ili kurejesha fedha husika, hata hivyo ilibainika kuwa malipo hayo hayakufanyika na kwamba maandalizi ya malipo hayo yalilenga kujibu hoja ya ukaguzi wa mwaka 2009/10.

Udhaifu Katika Ukusanyaji wa Mapato

Jumla ya kiasi cha Sh.7,117,500 kilikusanywa kupitia vitabu 23 vya kukusanyia mapato. Kiasi hicho hakikuingizwa kwenye rekodi (daftari la fedha) wala hakikukatiwa stakabadhi na mtunza fedha. Pia kiasi cha Sh. 314,613 zilizokusanywa kupitia vitabu saba (7) vya Mtunza Fedha hakikuwasilishwa Benki.

Kukosekana Udhibiti wa Hundi Zinazolipwa

Mfuko Mkuu ilikuwa na salio nakisi la Sh.5,101,932 Machi 11,2009 na Sh.2,692,679 Julai 02,2009. Akaunti ya Afya ilionesha kuwepo nakisi katika salio kwa kiasi cha Sh.7,992,449 (tarehe 21/12/09) na 4,466,331 (tarehe 26/5/010). Pia akaunti ya Elimu

Sekondari ilionesha kuwepo salio nakisi la Sh.515,470 tarehe 20/8/010.

Halmashauri ilikuwa ikifanya malipo zaidi ya salio la fedha lililokuwepo katika akaunti husika za Benki hivyo kuwajibika kulipa faini za kibenki (bank charges) kiasi cha jumla ya Sh.630,000.

Utaratibu mbovu wa Manunuzi

Zabuni kwa ajili ya kuwapata wakandarasi katika miradi ya ukarabati wa malambo vijiji vya Isamilo, Mwalogwabagole, Buganda, Isakamawe, Buhunda na Matale zilikiuka sheria ya manunuzi ya umma ya 2004.

Mzabuni M/s Karagwe Estate Ltd alipatiwa kazi kwa vijiji vyote kinyume na Kifungu Na.31(1)(b), Na.58(2) na Kifungu Na.73(1)(b) vya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya 2004.

Mikataba iliyoingiwa kati ya Mzabuni M/s Karagwe Estate Ltd na vijiji sita (6) haikujumuisha vipengele muhimu hali iliyotokana na ukosefu wa utaalum katika manunuzi ya Halmashauri za Vijiji.

Usimamizi Duni wa Idara ya Afya

Baadhi ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa za jumla ya Sh.206,152,770 hazikutekelezwa licha ya kupokelewa fedha zake. Hali hiyo imetokana na usimamizi duni wa shughuli za Idara ya Afya chini ya aliyekuwa Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya na uhusiano mbaya wa kikazi uliopo baina yake na watumishi wengine wa Idara ya Afya.

Usimamizi usioridhisha wa Miradi ya Ujenzi

Halmashauri ilitekeleza miradi ya ujenzi katika kipindi cha mwaka 2008/09 na 2009/10 ambayo haikusimamiwa kikamilifu. Miradi hiyo ilihusisha:

Jina la Mradi	Kiasi Kilicholipwa (Sh.)
Ujenzi wa Nyumba ya Mkurugenzi	50,000,000
Ujenzi wa Ofisi ya Mhandisi wa Maji	96,260,100
Ukarabati wa Jengo linalotumika sasa na Halmashauri	73,268,859
Ujenzi wa Matenki 13 ya Kuvunia Maji	154,114,600
Ukarabati wa Zahanati Tatu ³	93,946,326
Jumla	467,589,885

Ubadilishaji wa Matumizi ya Fedha kinyume na Utaratibu Sh.63,680,000

Kiasi cha jumla ya Sh.63,680,000 zilipokelewa na Halmashauri kwa ajili ya manunuzi ya magodoro, mashuka, mablanketi na chakula kwa ajili ya watoto wenye ulemevu wa Shule ya Msingi Mitindo kwa mujibu wa barua yenye Kumb.HB.116/285/01 ya Mei 08, 2009. Kiasi hiki kilibadilishwa matumizi yake na Mkurugenzi, kilitumika kugharamia ujenzi wa bwalo bila kufuata utaratibu na kutokupata kibali cha kubadili matumizi kutoka kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi ya Halmashauri.

Usimamizi Duni wa Mradi wa Ujenzi

Ujenzi wa Ghala katika kijiji cha Sumbugu Sh. 18,890,500 ulikuwa na mapungufu yafuatayo:

- Mradi ulitelezwa kwa muda wa takribani miezi kumi na nane (18) (tangu muda wa mkataba huo kuisha tarehe 25/01/2010 hadi muda wa ukaguzi) bila kutozwa tozo la kuchelewa kwa kazi; kipengele ambacho pia hakikuwekwa kwenye mkataba.
- Mkandarasi alisimama katika hatua ya jamvi kama inavyoonekana katika picha hapa chini

³ Koromije, Gambajiga na Mwawile



Picha ya Ghala la kijiji cha Sumbugu ukiwa katika hatua ya jamvi iliyochukuliwa tarehe.04/09/2011.

Ukarabati wa mfumo wa maji katika kijiji cha Usagara uliogharimu jumla ya Sh. 111,271,543 ulikuwa na mapungufu yafuatayo:

- Malipo ya Sh. 3,276,603 zaidi ya malipo stahili
- Manunuzi ya pampu hayakufanywa kwa ushindani kwa mujibu wa sheria bila sababu na hayakupata idhini ya Bodi ya Zabuni
- Utekelezaji duni wa kazi ambao ulipelekea kuta kutoa nyufa kama inavyoonekana katika picha hapa chini:



Picha ya ukuta wa kibanda cha pampu wenye nyufa (iliyopigwa tarehe.03/09/2011)

imisho

la ya
gumza na
Masuuli

Malipo yenye mashaka Sh.19,415,000

Nyaraka zilizopitiwa zilionesha kwamba Sh.19,415,000 zilitumika kugharamia shughuli za kutathmini Ujenzi na shule na mafunzo. Hata hivyo uhalali wa malipo hayo haukubainika kwa kukosekana viambatanisho. Baada ya uchunguzi zaidi kwa watendaji wa Halmashauri ilibainika kufunjwa kwa kiasi husika.

Mkurugenzi wa Halmashauri ameshindwa kutekeleza majukumu yake vizuri. Upungufu wa usimamizi juu ya mali, mishahara, akaunti za benki, miradi ya maji, miradi ya kilimo, miradi ya matenki ya maji, ujenzi wa majengo ya makazi kwa ajili ya Mkurugenzi, majengo ya ofisi ya Halmashauri na mahusiano ya kikazi.

Taarifa hii ya jumla ya ukaguzi pamoja na ripoti kamili ya ukaguzi maalum wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi zinapaswa kutumiwa na Wah.Madiwani wa Halmashauri ya Misungwi katika kuihoji Menejimenti ya Halmashauri juu ya hatua zilizochukuliwa katika:

- Watumishi waliojikusisha na vitendo vya ubadhirifu na usimamizi mbovu wa miradi.
- Kuhakikisha kuwa uhusiano mzuri wa kikazi kati ya Waheshimiwa Madiwani na watendaji wa Halmashauri unakuwepo.
- Kuboresha na kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani wa Halmashauri.



Ukaguzi wa Ufanisi


Sura ya 4

Mambo yanayo-hitaji kuzingatwa

Sura hii ni muhtasari wa masuala muhimu ambayo yamejitokeza zaidi katika kaguzi za ufanisi na kiuchunguzi hadi sasa. Lengo la sura hii ni kuanisha udhaifu unaojirudia katika kaguzi zetu unaohitaji serikali kuufanyia kazi.

Lengo la kufanya ukaguzi wa ufanisi ni kutoa taarifa juu ya uwekevu, tija na ufanisi kwenye matumizi ya rasilimali za umma wakati wa utekelezaji wa shughuli za serikali. Hata hivyo, kutokana na uchache wa rasilimali zinazohitajika ili kufanya ukaguzi wa ufanisi ni matarajio kuwa serikali itayachukulia kwa umakini masuala yaliyojitokeza katika kaguzi zilizofanywa ili kuhakikisha masuala hayo yanatekelezwa kwa tija na ufanisi katika taasisi nyingine za serikali.

Tangu mwaka 2007 hadi leo, kuna takribani ripoti kumi na moja (11) za ukaguzi wa ufanisi. Taarifa hizi zimejumuisha maeneo mbalimbali ya ukaguzi na kushirikisha wakaguliwa tofauti. Uchambuzi wa masuala ambayo yalijitokeza zaidi katika ripoti hizo ni kama ifuatavyo:



Hata hivyo, masuala hayo yanaweza kufafanuliwa kama ifuatavyo:

Udhaifu katika mifumo ya ufuatiliaji

Kukosekana kwa mifumo ya ufuatiliaji ni tatizo kubwa katika ngazi ya serikali kuu na za mitaa. Kwa mujibu wa uchambuzi uliofanywa, suala hili limejitokeza katika kaguzi zote 11 za ufanisi tulizozifanya hadi sasa. Ni jambo la kawaida kuona mipango mizuri ya uendesaji lakini utekelezaji hafifu kutokana na kuwepo kwa mifumo ya ufuatiliaji isiyokidhi. Kwa mfano, Serikali Kuu ambayo ina jukumu la kutunga sera na kuhakikisha utekelezaji wake unafanyika kikamilifu imeonekana kuwa na mifumo dhaifu ya ufatiliaji katika utekelezaji wa sera zilizotolewa.

Udhaifu katika mifumo ya kutathmini

Uchambuzi wa ripoti zote za ukaguzi wa ufanisi zilizotolewa, umeonyesha udhaifu katika kufanya tathmini. Taasisi zilizokaguliwa zinakosa viashiria fasaha na mahiri vya kupimia utendaji katika mipango ya shughuli zao ambavyo ndio msingi wa kufanyia tathmini. Maranyingi, tathmini inafanywa kupitia ripoti zinazowasilishwa kutoka ngazi ya chini ambayo inaweza isionyeshe hali halisi ya mambo yalivyo. Taasisi za serikali hazina mipango ya kufanya tathmini ambayo inaonyesha wakati na jinsi gani tathmini itafanyika.

Mapungufu katika miongozo

Udhaifu katika kutengeneza miongozo umejitokeza katika kaguzi sita zilizofanywa. Kwa hali hiyo, ilibainika kwamba baadhi ya maeneo hayakuwa na sera, miongozo wala viwango vinavyoongoza utendaji wa shughuli zao.

Kwa mfano, katika ripoti ya ukaguzi wa ufanisi wa matengenezo ya magari yanayomilikiwa na serikali, hakuna sera ya matengenezo ya magari wala miongozo ya kutosha inayofafanua jinsi gani matengezo ya magari ya serikali yatafanyika. Pia, katika ripoti ya ukaguzi wa programu ya ukaguzi wa shule za sekondari imegundulika kuwa hakukuwa na vipaumbele fasaha vinavyoelekeza jinsi programu hiyo ya kaguzi za shule inavyotakiwa kufanyika.

Udhaifu katika mawasiliano

Mfumo wa mrejesho kutoka ngazi ya juu ya mamlaka kwenda ngazi ya chini umeonekana kuwa na udhaifu katika kaguzi nane zilizofanyika. Kwa mfano, ripoti za utekelezaji zilizowasilishwa na Wakurugenzi wa Halmashauri kwenda Serikali Kuu hazikuwa na mrejesho. Pia katika ukaguzi wa programu ya ukaguzi wa shule iligundulika kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi haikuwasilisha taarifa ya matokeo ya ukaguzi uliofanywa kwa wadau muhimu. Vile vile, katika ukaguzi wa huduma za afya ya msingi, iligundulika kuwa Waganga wakuu wa halimashauri hawakutoa mrejesho kwa wakuu wa vituo vya afya juu ya taarifa zilizowasilishwa.

Upatikanaji wa takwimu/taarifa na mfumo ya usimamizi wa habari usiotosheleza

Hii pia ni miongoni mwa matatizo makubwa yaliyojitokeza katika kaguzi kumi zilizofanyika. Kuna udhaifu katika kuhifadhi kumbukumbu. Hakuna mfumo wa kuhakiki ubora wa taarifa zilizokusanywa. Mfumo wa kukusanyia taarifa hauboreshwi kwa wakati.

Kwa mfano, katika ripoti ya huduma ya afya ya msingi, mfumo wa kukusanyia taarifa (MTUHA) haukuboreshwa kuendana na wakati na kusababisha baadhi ya taarifa kukosekana. Vile vile, mfumo wa

kukusanya taarifa (NAFOBEDA) katika wizara ya Maliasili na Utalii hautumiki ipasavyo na kusababisha ukosefu wa baadhi ya taarifa kutoka katika mfumo huu. Pia katika ukaguzi wa kusimamia taka ngumu, lilionekakana tatizo la ukosefu wa taarifa zinazohusiana na kiasi cha taka ngumu kinachozalishwa.

Ukosefu wa vigezo fasaha vya mgawanyo wa rasilimali

Suala la kugawa rasilimali za serikali pia lilikutwa na udhaifu. Katika kaguzi tatu zilizofanyika, udhaifu ulikutwa katika mgao wa rasilimali watu, vifaa na fedha. Hii ilitokana na ukosefu wa vigezo fasaha vyakugawia rasilimali hizi katika shughuli mbalimbali za serikali. Kwa mfano, katika ripoti ya huduma ya afya ya msingi, vituo vya afya vilitengewa kiasi sawa cha fedha kwa ajili ya kununua dawa bila kujali wingi wa wateja katika kituo.

Vile vile, katika ukaguzi wa usimamizi wa uvunaji misitu, asilimia sitini (60%) ya vizuia vya wizara vimejengwa katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani wakati maeneo yenye hatari kubwa ya uvunaji haramu yalikuwa na vituo vichache.

Utekelezaji wa sheria na vikwazo usiotosheleza

Katika kaguzi nne za ufanisi zilizofanyika ilibainika kuwa utekelezaji wa vikwazo kama vile adhabu, faini na sheria nyingine hautoshelezi. Vikwazo havikutekelezwa ili kuhakikisha makosa hayajirudii.

Hii imejitokeza katika ukaguzi wa usimamizi wa taka ngumu ambapo hatua toshelezi hazikuchukuliwa kwa watoa huduma waliokiuka mkataba. Pia katika ukaguzi wa usimamizi wa utoaji kazi ya kukusanya mapato ya Halmashauri kwa mawakala, udhaifu ulikwepo katika utekelezaji wa vikwazo kwa

mawakala waliokiuka masharti ya mkataba. Vile vile, katika ukaguzi wa uvunaji wa misitu, vikwazo na adhabu kwa wahalifu havikuweza kuleta mabadiliko yaliyokusudiwa.

Udhaifu katika usimamizi wa muda katika utoaji huduma

Tatizo la muda limejitokeza katika kaguzi saba kati ya kaguzi kumi na moja zilizofanyika hadi sasa. Masuala ya muda yalijitokeza katika kushugulikia madai ya wastaafu, muda ulitumika katika kutoa huduma kwa wahudhuriaji wa vituo vya afya na muda uliotumika katika kutekeleza miradi ya ujenzi ulionekana kuvuka muda wa kikomo uliotarajiwa. Maranyingi sababu za tatizo hili ilikuwa ni kukosekana kwa ufanisi katika mchakato wa utoaji wa huduma.

Ukaguzi wa Kiuchunguzi

Kulingana na kaguzi zilizofanywa hadi sasa, kuna masuala muhimu ya kuzingatiwa na Serikali. Haya ni mambo ambayo yatakuwa na madhara kama hayo kwa taasisi nyingine kutokana na kutokidhi kwa mifumo ya udhibiti ya ndani kama ifuatavyo:

Udhaifu katika udhibiti wa kimazingira

Ilibainishwa katika kaguzi zilizofanyika kuwepo kwa matukio ambapo taasisi imeonyesha kutokuwepo kwa mawasiliano stahili na ya wazi yenye ufanisi kama njia ya kuwapatia taarifa muhimu mameneja juu ya vitendo vya kibadhirifu.

Tathmini ya uwezekano wa kutokea ubadhirifu

Katika baadhi ya kesi ilibainika kuwa tathmini ya uwezekano wa kutokea vitendo vya kibadhirifu ilifanywa na wakaguzi wa ndani katika hatua ya kuandaa mpango wa ukaguzi. Tathmini hiyo ilifanyika kwa kuzingatia mpango mkakati wa ukaguzi wa ndani, hivyo kulenga wigo wa ukaguzi wa ndani pekee. Hata hivyo, zoezi halikushirikisha wafanyakazi watendaji wala halikuzingatia shughuli zinazotekelezwa.

Upungufu katika miongozo ya kubaini udanganyifu

Ilibainika kutokuwepo kwa taratibu rasmi za kimaandishi zilizowekwa ili kubaini, kuchunguza na kudhibiti dalili zozote za udanganyifu. Sera ihusuyo tathmini juu ya uwezekano wa vitendo vya ubadhirifu na hati mkakati ya kimaandishi havitoi miongozo kwa kazi za kiuchunguzi zinazofanyika.

Kukosekana ufanisi katika habari na mawasiliano
Ilibainika kuwa baadhi ya taarifa kuhusu sera ihusuyo vitendo vya ubadhirifu hazikuwasilishwa kwa ufanisi kwa wafanyakazi, pia ilibainika kwamba hakukuwa na vipaumbele vilivyotolewa kwa watumishi watendaji.

Ufuatiliaji usioridhisha

Ilibainika katika kesi za awali kwa baadhi ya taasisi kuwa hakukuwa na taratibu zenye kuleta ufanisi kwa ajili ya ufuatiliaji na kuona iwapo mfumo wa sheria uliopo unatekelezwa kama ilivyokusudiwa. Hayo ni matokeo ya asili kwa kuwa hakukuwa na hatua za kudhibiti mienendo/tabia katika taasisi. Hii ina maana kwamba si rahisi kufuatilia jambo lisiloweza kulinganishwa.

Mikataba kutokuwa na vipengele muhimu

Ilibainika kwamba baadhi ya mikataba iliyoingiwa na taasisi za serikali haikujumuisha vipengele muhimu kama njia ya kuhakikisha kuwa kila upande unatimiza wajibu wake. Hivyo, ukiukwaji mkubwa wa wajibu umewezekana kwa kutokuwepo vipengele muhimu katika mikataba hali ambayo imechangia kutofikiwa kwa malengo ya mikataba husika.

Ukiukwaji wa taratibu za manunuzi

Sheria zinazotawala manunuzi ya umma zinapaswa kuzingatiwa na taasisi za serikali ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinazonunuliwa zinakidhi ubora na malengo. Ilibainika kuwa maombi ya kufanyika kwa baadhi ya manunuzi yaliyofanyika hayakutolewa na watumiaji husika wala hayakuwa yamebainishwa. Pia ilibainika kuwa baadhi ya manunuzi hayakuthibitishwa na Bodi ya Zabuni.

Udhaifu katika usimamizi wa mikataba

Kwa ujumla umejitokeza udhaifu mkubwa katika kusimamia mikataba inayoingiwa kati ya Serikali (Kuu na Halmashauri) na taasisi za sekta binafsi. Mikataba mingi iliyoingiwa ilitengenezwa katika hali isiyoinufaisha Serikali.

Kwa kuhitimisha, uchambuzi umeonyesha kwamba Serikali inapaswa kuchukua hatua kali juu ya udhaifu na mapungufu ambayo yameonekana kujitokeza zaidi katika shughuli za Serikali (Kuu na Halmashauri). Matokeo, hitimisho, na mapendekezo juu ya udhaifu na mapungufu vinapaswa kuchukuliwa kama angalizo kwa taasisi nyingine za serikali ili kuboresha utekelezaji wa shughuli zao.



Sura ya 5

**Maeneo
ya
kuzinga-
tia katika
kaguzi
zinazo-
kuja**

Ukaguzi wa Ufanisi

Lengo la Ofisi ya Taifa ya ukaguzi wa Hesabu za Serikali ni kulisaidia Bunge katika kutekeleza majukumu yake na pia kusaidia kuboresha utendaji na uwajibikaji wa serikali kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania.

Katika kipindi kijacho Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ina mpango wa kulenga masuala yafuatayo:

1) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika kaguzi zilizopita.

- Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali itafuatilia mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa tatu za ukaguzi wa ufanisi ambazo zilijadiliwa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali ili kuona utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na kamati ya Bunge kwa Maafisa Masuuli katika kusahihisha mapungufu yaliyobainishwa.
- Pia, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali itachukua hatua madhubuti ili kuhakikisha kwamba taarifa za ukaguzi wa ufanisi zilizokwisha wasilishwa Bungeni zinajadiliwa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC).

2) Mapendekezo ya maudhui ya kaguzi zijazo

Ili kupata matokeo makubwa kutokana na kazi ya ukaguzi wa ufanisi, mkazo utawekwa zaidi katika utendaji wa sekta ya umma ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa mapendekezo yanayotolewa kwenye taarifa za kaguzi za ufanisi. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeainisha pia maudhui ambayo yatatoa mwelekeo wa kazi ya ukaguzi wa ufanisi na kusaidia pia katika uchaguzi wa kaguzi zijazo. Maudhui hayo

yanahusu masuala muhimu katika utendaji wa sekta ya umma. Yafuatayo ni maudhui yaliyoainishwa:

- **Ukaguzi wa bajeti ya Serikali:** kufuatia umuhimu wa bajeti katika kuongeza ukuaji endelevu wa uchumi, mkazo utakuwa kwenye eneo mojawapo katika mchakato wa kuandaa bajeti ya Serikali.
- **Usimamizi wa mikataba:** usimamizi wa mikataba mbalimbali ya serikali utaangaliwa.
- **Ukaguzi wa Mazingira:** kupitia masuala ya madini ili kuona hatua zinazochukuliwa na serikali kuhusu masuala ya madini na uharibifu wa mazingira.
- **Utoaji wa huduma:** vyombo vya serikali vina jukumu la kuhakikisha ubora na gharama nafuu za utoaji wa huduma ili kukidhi matarajio ya Bunge, serikali na jamii.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi itaendelea kuchunguza na kujadili na wadau mbalimbali juu ya maudhui ya kaguzi zilizoainishwa kuona kama na jinsi maudhui yaliyopendekezwa yanavyoweza kutumika kukuza utawala bora katika uendesaji wa serikali. Ofisi imepanga kuandaa mpango mkakati wa ukaguzi wa ufanisi ambao utaelezea malengo na mikakati iliyopendekezwa katika kulisaidia Bunge na taifa kwa ujumla kuboresha utawala nchini.

Ukaguzi wa Kiuchunguzi

Imeonekana kwa miaka miwili iliyopita kuongezeka kwa idadi ya matukio ya udanganyifu katika taasisi nyingi za umma; hali ambayo pia imechangia kuongezeka zaidi kwa mahitaji ya kaguzi maalum ambazo ofisi imekuwa ikizifanya kwa wingi hivi karibuni. Kama sehemu ya kushughulikia hali hii tuna nia ya kuelekeza ukaguzi wetu wa kiuchunguzi kwenye maeneo yenye udhaifu ambayo yamejionesha zaidi katika kaguzi nyingi maalum zilizofanywa.

Maeneo ambayo yamedhihirika katika kaguzi maalum ambayo tuna nia ya kuyazingatia katika mwaka ujao ni pamoja na; uchunguzi katika maafikiano ya siri (collusions) juu ya mikataba inayoingiwa, ubadhirifu wa mali, mipango ya udanganyifu katika hundi na matumizi mabaya ya ofisi za serikali. Kulenga katika maeneo yalioainishwa hatimaye kutasaidia kuzuia kutokea kwa ubadhirifu, kuongeza uwajibikaji katika rasilimali za umma.

Tuna nia ya kuimarisha mshikamano uliopo kati ya ofisi na vyombo vya sheria kwa lengo la kuhakikisha kuwa kuna ushirikiano mzuri kati ya ofisi hizi. Pia, masuala yaliyohojiwa wakati wa ukaguzi kupewa kipaumbele sahihi pia kwa upande mwingine unaohusika na mchakato wa mashitaka.

Kulingana na maandiko mbalimbali⁴ imefahamika kuwa upashaji taarifa za siri 'tips' ni njia bora zaidi ya kugundua shughuli za udanganyifu kama hatua ya awali. Jambo muhimu sana kufanyika kwa ajili ya

⁴ - Ripoti ya Kitaifa (Jarida la mwaka la ACFE) 2008 na la 2009.
- Jarida la ACFE (Jarida la Robo Mwaka) la Desemba 2011

kupokea ‘tips’ ni kujenga mazingira ya siri kwa wapashaji wa taarifa hizo za siri kutoa ‘tips’. Vile vile, tuna mipango ya kuanzisha huduma ya simu ‘hotline’ kwa ajili ya ofisi ambayo inaweza kutumika kwa ufanisi kwa kukusanya ‘tips’ ambazo zitafanyiwa uchambuzi kabla ya ukaguzi.

Kiambatanisho

Jedwali la uchambuzi wa maswala 10 ya msingi katika taarifa 11 za ukaguzi wa ufanisi zilizofanyika katika kipindi cha 2007 - 2012

Taarifa ya ukaguzi	Ufuatiliaji	Tathmini	Mgawanyo wa rasilimali	Miongozo	Mawasiliano	Upatikanaji wa takwimu na mfumo wa taarifa	Utekelezaji wa sheria	Muda
Mafuriko	Ufuatiliaji wa maofisa katika kutengeneza Mipango ya maafa inayotakiwa	Mafuriko yametokea bila kufanya tathmini endelevu ya vihatarishi	X	X	X	Ofisiya Waziri Mkuu-Kitengo cha Maafa hakina rejesta ya maafa kwa zaidi ya miaka 10	X	Mamlaka za serikali za mitaa zinachukua muda mrefu kukarabati miundombinu baada ya mafuriko
Ukaguzi wa shule	Ufuatiliaji katika kushughulikia maswala yanayosababisha kushindwa kwa wanafunzi katika hisabati na masomo ya sayansi	Upungufu wa tathmini ya utendaji wa shule	X	Ukosefu wa mwongozo wa vitendo kwa ajili ya wakaguzi	Matokeo ya uchunguzi na ukaguzi hayawasilishwi vizuri kwa wadau	X	X	X
Afya ya msingi	Timu za mkoa za usimamizi wa afya pamoja na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hazifuatili utendaji wa halmashauri katika kukagua utendaji wa vituo vya afya	Tathmini chache zilifanyika juu ya mgawanyo wa rasilimali katika vituo vya afya	Mgawanyo wa fedha za madawa, rasilimali watu na vifaa hauzingatii ukubwa wa kazi katika vituo vya afya	X	Wakuu wa vituo vya afya hawapati mrejesho kutoka kwa afisa afya wa wilaya	Mfumo wa taarifa ya usimamizi wa afya haukuweza kupata takwimu kutoka katika ngazi ya chini	x	Muda mrefu unatumika kuwahudumia wageni katika vituo vya afya
Ujenzi wa barabara	Upungufu wa taaluma na uadilifu katika ufuatiliaji wa miradi ya ujenzi wa barabara	Tathmini zilizofanyika hazikuweza kugundua baadhi ya udhaifu katika ujenzi wa barabara	X	Maelekezo yasiyotosha kutoka Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu	Mikataba ya mradi wa ujenzi wa barabara haiwekw wazi kwa umma	Hakuna mfumo sahihi wa kurekodi utendaji wa wakandarasi	faini zinazotakiwa kutozwa kwa kutowastish a kazi kwa wakati	Kupitiliza kwa muda uliopangwa kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara

Taarifa ya ukaguzi	Ufuatiliaji	Tathmini	Mgawanyo wa rasilimali	Miongozo	Mawasiliano	Upatikanaji wa takwimu na mfumo wa taarifa	Utekelezaji wa sheria	Muda
				kwa Wakala wa Barabara Tanzania kuhusu jinsi ya kusimamia washauri			hazitekelezwi ipaswavyo	
Taka ngumu	Tawala za serikali za mitaa hazifuatili kwa kiasi cha kutosha kazi zinazohusu taka ngumu	Serikali Kuu haijuhusishi kwa kiasi cha kutosha katika tathmini ya shughuli za taka ngumu	X	Ukosefu wa miongozo na viwango sahihi kwaajili ya usimamizi wa taka ngumu	X	Ukosefu wa mfumo unaoweza upatikanaji wa takwimu za taka ngumu zilizozalishwa katika vyanzo	Mamlaka za Serikali za Mitaa hazitoi adhabu kwa wanaovunja sheria	Taka ngumu hazikusanywi kwa wakati
Mafao kwa wastaafu	Upungufu wa shughuli za ufuatiliaji wa mafunzo na ufahamu	Upungufu wa ufuatiliaji wa programu za mafunzo	X	Hakuna miongozo ya sera iliyoandikwa kwaajili ya kuandaa na kupitia maombi, haki na rufaa	Mawasiliano mabaya kati ya wanahisa, mfuko wa pensheni, na waajiri	Utunzaji mbovu wa kumbukumbu na ucheleweshwaji wa kumbukumbu za wafanyakazi	X	Muda mrefu wa kuandaa mafao
Afya ya uzazi	Ukosefu wa Mipango ya ufuatiliaji wa kina kuhakikisha hatua za kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi zinatekelezwa	Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii haifanyi tathmini ya mara kwa mara ya vipengele muhimu vya afya ya uzazi	Rasilimali kwaajili ya afya ya uzazi ziliwekwa katika kundi moja na rasilimali za huduma zingine za afya badala ya kutenganishwa	X	Mawasiliano yasiyo na ufanisi baina ya timu ya mkoa inayosimamia afya (RHMT) na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (MoHSW)	Habari zisizo za uhakika kutoka katika mfumo wa taarifa za usimamizi wa afya		x
Ukusanyaji wa mapato	Kukosekana kwa ufuatiliaji kutoka mamlaka za juu katika kuhakikisha Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinafanya vizuri kwenye ukusanyaji wa mapato	Taarifa za fedha kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa hazifanyi tathmini na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI (PMO-RALG)	X	X	Mamlaka za juu hazitoi mrejesho kwa ngazi za chini	Ukosefu wa takwimu zilizokusanywa kutoka kwa wokusanyaji mapato	Hakuna adhabu endapo ziada inakusanywa lakini kinachopele kwa halmashauri ni kidogo	X
Usambazaji wa maji	Ukosefu wa viashiria vya utendaji kwaajili ya ufuatiliaji	Hakuna tathmini iliyofanywa juu ya mifumo ya mtandao wa maji	X	X	X	Mapitio ya taarifa hayafanyiki vya kutosha		Inachukua zaidi ya saa 24 kushughulikia matukio ya dharura

Taarifa ya ukaguzi	Ufuatiliaji	Tathmini	Mgawanyo wa rasilimali	Miongozo	Mawasiliano	Upatikanaji wa takwimu na mfumo wa taarifa	Utekelezaji wa sheria	Muda
Uvunaji wa misitu	Wizara ya Maliasili na utalii haifuatili shughuli za uvunaji wa misitu	Ukosefu wa tathmini ya mipango ya usimamizi wa misitu na utendaji wa viziua na vikosi vya doria	60% ya viziua vipo mikoa ya Dar es Salaam na Pwani	Ukosefu wa mwongozo sahihi kwa ajili ya kutathmini ubora na utekelezaji wa mipango ya usimamizi wa misitu	Hakuna maoni kutoka MNRT kwenda kwa maofisa misitu wa wilaya juu ya taarifa zilizowasilishwa kwao kuhusu uvunaji	Takwimu kutoka orodha ya Taifa ya Misitu na nyuki (NAFOBEDA) si ya kuaminika	Faini na adhabu hazina njia iliyokusudi wa kuzuia madhara	X
Magari yanayomilikiwa na Serikali	Ukosefu wa Mipango ya ufuatiliaji wa gereji binafsi	Hakuna tathmini iliyofanyika	X	Ukosefu wa sera ya matengenezo	Mawasiliano mabovu miongoni mwa taasisi za serikali zilizokabidhiwa usimamizi wa magari ya serikali	Hakuna rejesta ya hivi karibuni ya magari ya serikali	X	X
Pointi	11	11	3	6	8	10	4	6

Kielelezo:

X- haipo

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Maadili yetu

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi - Tanzania, kama Taasisi Kuu ya Ukaguzi, ni Mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi (INTOSAI)

Tuna kanuni za maadili zinazoongoza kaguzi zetu za kila siku. Aidha watumishi wana wajibu wa kutekeleza kanuni za Utumishi wa Umma na mwenendo wake na kanuni za maadili za taaluma zao.